# *KUHESABU KINYUMENYUME*

Asante, Ndugu Neville. Bwana akubariki.

Kwa namna fulani ni haraka kila mara. Nimeingia tu. Ndugu Moore alinipigia simu kuhusu kuja kule kwa yubile yao ya miaka hamsini ya Kipentekoste. Nilikuwa nikijaribu kupanga tarehe na Wafanyabiashara kule mahali pengine, nami nikasema. . . akainua simu, akasema, "Unasikia hiyo 'Amini Tu'? Unajua maana yake." Nami nikamwelekeza kwa Billy, na kukimbia kutoka mlangoni. Kwa hiyo si—sijui watatokaje huko nyuma, lakini ndivyo. . . Ninapenda sana kwenda Louisiana, hata hivyo, kwa watu hao, hao wazee wazuri wa Kusini chini kule. Lakini basi nilipaswa kuwa karibu na tarehe hizo hizo huko—huko Florida, kwenye mkutano wa eneo la Wafanyabiashara, na inafanya kuwa ngumu unapojaribu kuziunganisha kwa muda mfupi kama huo.

2 Sote tuna furaha kuwa hapa asubuhi ya leo, na kuwa hai na—na miongoni mwa wanaoweza kusema "Amina." Hiyo ni kweli. Sasa, nasikitika kwamba tumesongamana kabisa hapa ndani. Naye alisema baadhi ya watu walikuja na kuondoka tu kwa gari. Lakini sisi ni. . . Ndivyo vizuri zaidi tuwezavyo kufanya wa—wakati huu. Wajua. Mnaelewa, nina hakika. [Ndugu Branham anakohoa—Mh.] Samahani.

Je, mnaweza kusikia vizuri zaidi kutoka kwa *hii* au kutoka kwa *hii*? *Hii* hapa? Sawa, ilete tu hapa ili niwe karibu. [Ndugu Neville anasema, "*Hii* inafanya kazi. *Hiyo* ni—*hiyo* ni maikrofoni ya kurekodi."—Mh.] *Hii*, kurekodi hapa. Sawa. Sawa, bwana.

3 Je, mlifurahia jana usiku? Mimi. . . hakika tuliipata, na Bwana akatubariki. Mambo mengi tu zaidi yangeweza kusemwa kuhusu Ujumbe pale, lakini nilifikiri labda mngeweza kuisoma, mnajua, nanyi mtatambua, na katikati ya mistari, saa tunayoishi. Tuko moja kwa moja kwenye wakati wa mwisho. Nami ninaamini hilo. Bila shaka, kila mtu amefikiria hivyo, nadhani, tangu Yesu alipoahidi kurudi. Lakini, unajua, moja ya siku hizi Yeye atakuja, hata hivyo, unaona. Kwa hivyo sioni chochote kilichosalia kutokea, ila tu kunyakuliwa kwa Kanisa.

4 Sasa, kabla tu hatujaukaribia Ujumbe ninaotaka asubuhi ya leo, juu ya somo la *Kuhesabu Kinyumenyume*. Na sasa sisi. . . na usiku wa leo, kumbuka ibada ya usiku wa leo sasa, ni *Kuishi Katika Uwepo Wake*. Unaona? Na tutajaribu kufanya haraka, kuharakisha, ili uweze kuondoka ili tuweze kuanza kazi tena Jumatatu asubuhi. Na tunashukuru kwa ajili yenu nyote. Sijui tungefanya nini, ningefanya nini bila nyinyi. Mimi tu—singeweza kabisa kuendelea bila nyinyi.

5 Na ninataka kutoa shukrani za pekee kwa huyo Dada Williams, nadhani hata simjui mwanamke huyo. Nilipoamka asubuhi ya leo, jamani, Ndugu Charlie Cox alikuwapo, na—na—mlangoni kulikuwa kumejaa chakula, bidhaa za makopo na kadhalika. Jinsi maskini mwanamke huyo lazima alitokwa na jasho wakati wa kiangazi hiki, akiweka vitu hivyo kwenye makopo, nyanya na vyakula. Sasa, hiyo ina maana kubwa sana kwangu. Na Dada Williams, ninaamini waliiacha Biblia yako pale ili iombewe, ikasemwa uombe kwamba Mungu ataninii . . . Niliomba asubuhi ya leo chumbani nilipokuwa nasoma kwa ajili ya Ujumbe, kwamba Mungu angechukua yaliyomo katika Biblia hiyo na kuyaweka moyoni mwako. Nami ninaomba kwamba Mungu akubariki. Laiti ningeweza kukulipa kwa hilo, dada, najua hakika ulipitia mengi ya kutokwa na jasho hilo. Nami ninakushukuru sana! Ni kidogo sana kusema, lakini hebu niwape Maandiko ambapo tunajua, kama nilivyosema jana usiku, halitashindwa. Yesu alisema, "Kadiri ulivyowafanyia hawa wadogo . . . " huyo angekuwa mimi, ona, " . . . walio wadogo kabisa katika hawa watoto Wangu, umenitendea Mimi." Hebu na irudi kwako jinsi tu ingekuwa kama ungeikabidhi moja kwa moja mikononi Mwake. Mungu akubariki kwa hilo.

6 Asanteni nyote. Mkiwa hapa, naona kwenye za—zaka na vitu mnavyolipa, hiyo ni imani yenu kwetu, ya kwamba vitaenda kwa ajili ya Ufalme wa Mungu. Sasa, tunawajibika kwa jambo hilo, unaona, na hatuna budi kutoa hesabu kwa ajili yake. Kwa hiyo tunataka kuangalia kila kitu tunachofanya, kufanya kila hatua kuwa kamilifu tuwezavyo, jinsi Bwana wetu angetaka, kwa sababu hatujui ni saa ngapi atatuita ili kujibu na kisha tutoe hesabu kwa kila kitu ambacho kimetujia.

7 Hiyo ndiyo sababu ninafikiri Paulo, jana usiku, alikuwa na koti moja tu. Unaona? Angeweza kuwa na zaidi, lakini hakuwa nayo. Hilo ndilo koti moja pekee ambalo angeweza kutumia kwa wakati mmoja, kwa hiyo aliliweka tu hilo. Sidhani kama alijali utajiri wa dunia. Sidhani kama alijali umaarufu, mnajua ninalomaanisha, kila mtu katika mienendo yao mikuu ya kidini kama ilivyo leo. Na watu wengi sana . . .

8 Najua hii inarekodiwa. Na ninaposema mambo hapa, ninatambua kwamba sizungumzi na kusanyiko hili tu, bali ulimwenguni kote. Na mimi . . . Kwa sababu kanda hizi zinaenda katika mataifa mengi, mengi, na wanazipeleka hata huko katika makabila huko Afrika, huko nyuma, na kuketi huko, na mhudumu anaichukua na kuzifasiri kanda hizo kwa watu, huko nyuma ambapo hawajui hata mkono wa kulia na wa kushoto ni upi. Unaona? Mbali kabisa kuingia Australia na kupitia huko ambapo watu ni—ni, hata . . . Kitu pekee wanachokula ni . . . Jinsi wanavyopata sukari ni kuchukua ganda kidogo na kuchimba kundi la mchwa na kung'ata mgongo wao namna hiyo. Hivyo ndivyo wanavyokuwa kwenye kupata sukari yao. Na

hawana nguo, hawana chochote. Wanamchukua kangaruu mzee na kumtupa juu ya moto, matumbo ndani yake, matumbo na kila kitu, na kumchoma kidogo kisha wanamla. Na ndivyo hivyo, ni ya kutisha. Na kumbukeni, kanda hizi zinachezwa huko nyuma. Ujumbe mnaousikiliza hapa unachezwa huko nyuma, na mamia ya wamishenari wakichukua kanda hizi na kuzicheza huko nyuma, na kuzifasiri kwa watu. Kwa hiyo, unaona, nitakapofika kule kwenye Siku ya Hukumu, unaona kile kitakachokuwa juu ya mabega yangu? Vipi kama nikimpotosha mtu? Unaona? Haya basi. Hebu wazia tu moja ya nafsi hizo, kama ningewapotosha kwenye jambo baya.

9 Kwa hiyo ninao hapa ndugu zangu katika mashirika haya. Na wengi wao ni watu wazuri, wengi wao, ninafurahia jambo hilo. Lakini baadhi yao huwa. . .na kwa kawaida viongozi hufika mahali ambapo inabidi wajifunge na kuifanya iwe kama, loo, kama jambo la kisiasa. Wanaingiza siasa ndani yake. Na, katika hilo, wanatoka kwenye Neno la Mungu.

10 Nami sina budi kubaki kwenye Neno. La—lazima nibaki hapo. Nayo ni lazima tu ifikie hili. Na mimi—mimi—mimi lazima niende nayo tu, hakuna lingine. Kwa hivyo, na sisi ni. . .Unajua, huwa tunaimba wimbo mdogo, "Tunaelea chini kwenye mkondo wa wakati, hatuna muda mrefu wa kukaa." Mmeusikia. "Mawingu ya giza yenye dhoruba yatageuka kuwa mchana angavu zaidi." Hiyo ni kweli. "Hebu sote tujipe moyo, kwa maana hatujaachwa peke yetu." Hiyo ni kweli. "Mashuaokozi hivi karibuni inakuja kupeleka Vito Nyumbani." Huo ndio wakati ambapo ninatazamia basi kuwa na koti ambalo halitachakaa kamwe, ndilo hilo, lile la Milele. Nami sina budi kuwa mwaminifu kwa Mungu, bila kuzingatia mambo hapa duniani, mpaka tutakapofika kule. Na kisha tutaweza. . .hilo ndilo litakalodumu.

11 Kwa hiyo mimi, katika hii thelathini. . .nikiendelea miaka thelathini na miwili ya huduma, nimejaribu kudumu mwaminifu kwa Neno. Sijui hata kitu kimoja ambacho kimenibidi kubadilisha, kwa sababu niliisoma tu kutoka katika Biblia, nikasema vile tu Biblia ilisema, na kuiacha iende hivyo. Na kwa hivyo sikulazimika kurudisha au kupanga upya, kwa maana nilisema tu jinsi Biblia inavyosema. Pia, naona, kama Mungu amesema jambo lolote, basi hatuna budi kuambatana na Neno hilo ili kulifanya litimie. Tumeona jambo hilo, kama nilivyowaambia jana usiku, juu ya ono hivi majuzi tu, unaona, kwamba hilo. . .Ilibidi niwepo, na onyo liwepo, na kuniambia miezi sita kabla ya kuwa mahali hapo, na kusimama hapo na kusema, "Nenda huko chini" (mara tatu) "pamoja nao." Nami niliendelea tu kutembea na wanaume wengine. Na lile ono likapita moja kwa moja, sehemu ya Mungu, nami nikaachwa nimesimama. Kwa hiyo tunataka kukumbuka, huna budi kukaa kwenye Neno, kudumu tu na Neno moja kwa moja. Na pale

Neno linapoongoza, wewe nenda moja kwa moja na Neno, nalo litakuvusha salama, nina hakika.

12 Sasa, najua mmekuwa hapa ndani tangu saa mbili, na labda ni saa nne sasa hivi. Ndivyo. Basi hebu tuombe sasa kwa Bwana wetu. Je, kuna haja zozote maalum? Ninaona leso nyingi zimewekwa hapa. Inueni mikono yenu kwa ajili ya haja hizo. Mungu awabariki. Sasa Yeye . . . Nimemjua kwa muda mrefu vya kutosha kujua hili, kwamba Yeye huona kila mkono na anajua kila moyo, na jambo pekee lililosalia kufanya ni kumwomba tu. Nawe unaamini, na inafanyika. Sasa, amininі tunapoomba.

13 Baba wa Mbinguni, sasa tunakikaribia Kiti kikuu cha Enzi cha Mungu, kama wanadamu katika mwili wa kawaida, hata hivyo sauti zetu zikinena maneno yanayokuja katika hicho Kiti kikuu cha Enzi mahali fulani katika awamu zingine ambapo Mungu anakaa. Kwa sababu, Yesu alisema, "Mkimwomba Baba lolote katika Jina Langu, nitalifanya." Na akatutaka tusiwe na shaka, lakini, tunapoomba, kuamini kwamba tunapokea kile tunachoomba, na tutapewa. Akasema, "Hata ungeweza kuuambia mlima huu, 'Ng'oka,' wala usiwe na shaka moyoni mwako, bali uamini ya kwamba uliyosema yatatimia, na yatakuwa yako yale uliyosema." Baba, tunajua kwamba hiyo ni kweli kabisa. Tunaitazama siku baada ya siku, na hakuna kosa katika Neno Lako. Ni kwa sababu hatuwezi kufika mahali hapo, wakati mwingine imani yetu haitatusogeza huko, tunafadhaika na kuwa na shaka. Lakini, asubuhi ya leo, tunajaribu kuja, Bwana, tukiwa na tumaini jipya, tukishikilia kambaokozi ya Kristo na ahadi Yake. Nasi tunakuja katika Uwepo wa Mungu kupitia Jina la Yesu.

14 Bwana, nina hakika ya kwamba Wewe unajua haja zote zilizofanywa zijulikane chini ya mkono ulioinuliwa asubuhi ya leo. Wangu pia uliinuliwa, na daima umeinuliwa Kwako, Bwana, kwa sababu mimi ni mhitaji. Nami naomba ya kwamba utatujalia kila haja. Waangalie, Bwana, na kuyajibu maombi yao, kuanzia mdogo zaidi hata mkubwa kuliko wote, kuanzia haja iliyo ndogo zaidi hadi haja kuu zaidi. Ndipo, Baba, uwajibu, kila mmoja. Ninaomba katika Jina la Yesu. Halafu ukumbuke yangu, Bwana.

15 Nami naomba na kukushukuru Wewe kwa kutupa mapumziko mema katika miili yetu, na kwa ujuzi tulio nao wa Neno Lako, na ufahamu tulio nao wa Roho, na daima tukiomba kwamba utupe ufahamu mkuu zaidi ili tusiwe watu bure, wenye kujivuna kwa hilo, bali watu wanyenyekevu, ili Roho Mtakatifu aweze kututumia kulitimiza Neno la Mungu, na kutuweka mahali hasa tunapohitajika kuwa saa hii. Kwa maana lazima tuwe mahali panapostahili ili itendeke. Nasi tunataka kuwa, Bwana. Ikiwa ni mke wa nyumbani nyuma ya meza, ikiwa ni kwa ajili ya m—mtu wa kiwandani aliye na spana mkononi mwake, na ushuhuda, ikiwa ni kwa ajili ya mhudumu mimbarani, au

shemasi au mdhamini, au kwa ajili ya mtoto shuleni, tineja katika majadiliano darasani, popote pale, Bwana, jalia tuwe hapo kwa wakati ufaao. Kwa maana tunajua Wewe umeahidi jambo hilo, na litatukia kwa sababu Wewe ulisema hivyo, na, mbona, ni imani yetu imejengwa pale.

16 Sasa, Bwana, tunahisi kwamba hatuna muda mrefu zaidi. Wakati unakuja. Tunaweza kuhisi ukungu kutoka anga za juu, unapoingia ndani. Tunajua kwamba hukumu na ghadhabu ya Mungu iko tayari kuanguka. Tunaweza kuhisi athari zake tayari. Nasi tunaomba, Bwana, ya kwamba utatusaidia.

17 Na sasa nisaidie, Bwana, juu ya Ujumbe huu mdogo asubuhi ya leo, wa kama dakika thelathini, unaoitwa *Kuhesabu Kinyumenyume*. Tusaidie, Bwana, kuelewa pale tulipo hasa.

18 Na ututakase sasa, Bwana, ukiondoa dhambi zetu na makosa yetu. Na kusiwe na mtu mmoja hapa asubuhi ya leo, aliyepotea, kila mtu na awe tayari, awe katika mduara huo mkuu tutakapokutana upande ule mwingine. Wakati majina yatakapoitwa, jalia nisikie jina baada ya jina, "niko." Hilo ndilo tunalotazamia, Bwana. Na wazee watakuwa wachanga huko milele, watabadilishwa kwa dakika moja, wasiopatikana na mauti, tutasimama kwa mfano Wake, kung'aa zaidi ya jua na nyota, kama Danieli alivyosema, "Wale walioelekeza wengi kwenye haki watang'aa kama nyota milele." Lakini tunasikia uliyomwambia nabii, "Nenda zako, Danieli, kwa maana utastarehe katika kura yako, lakini siku hiyo utasimama."

19 Ee Mungu, na tuhesabiwe tumestahili kwa Damu ya Yesu, hakuna sifa zetu wenyewe tunazodai, lakini kwa sifa Zake na tustahili kusimama katika siku hiyo tunapoungama makosa yetu na kutamani kusimama katika haki Yake, pamoja na nabii mkuu Danieli na wale wote watakaosimama thawabu zitakapotolewa. Mpaka wakati huo, Bwana, tufanye vyombo mkononi Mwako. Fanya masikio yetu vyombo asubuhi ya leo vya kusikia Neno. Ifanye midomo yangu iwe vyombo vya kulinena. Kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu, na jalia ufahamu wetu uelewe mapenzi ya Mungu. Amina.

20 Ni vigumu sana kuanza. Inaonekana kuna mengi sana ungeweza kusema na—na kutaka kusema, na inaonekana kama kuna muda mfupi sana wa kuyasema. Labda kabla ya mimi—mimi kuondoka. Nilisema jana usiku, tunaweza kupata nafasi la—labda kupitia moja ya Vitabu vya Biblia, wakati huu wa mapukutiko au msimu wa baridi, kabla ya kuondoka. Nikienda, ninataka kwenda ng'ambo, Bwana akipenda, mara baada ya Krismasi wakati fulani.

21 Sasa nawataka mfungue asubuhi ya leo kwa ajili ya usomaji, kwenye Waebrania mlango wa 11. Na sasa sikilizeni kwa makini sana usomaji. Nataka ku—kusisitiza juu ya kifungu cha 3.

*Basi imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana.*

*Maana kwa hiyo wazee walipata ushuhuda mzuri.*

*Kwa imani twafahamu ya kuwa ulimwengu uliumbwa kwa neno la Mungu, hata vinavyoonekana havikufanywa kwa vitu vinavyoonekana.*

22 Sasa, hilo kidogo ni kifungu kisicho cha kawaida kwa msingi wa somo ambalo na—nataka kutumia. Vitu havikufanywa kwa vitu vinavyoonekana. Sasa nataka kutumia somo hili asubuhi ya leo, *Kuhesabu Kinyumenyume,* kwa sababu ninataka kufanya u—ulinganishi kwa njia ya unabii. Jana usiku nilitaka kufundisha kidogo juu ya Maandiko; asubuhi ya leo Ujumbe wa kinabii; na usiku wa leo Ujumbe wa kiinjilisti.

23 Sasa, vitu ambavyo vilifanywa kwa vitu ambavyo havionekani. Sasa, nimejifunza katika miaka hii yote kwamba mambo yote ya asili ni mifano ya mambo ya kiroho, kila kitu kilicho katika asili. Na sasa kumbuka tu, ya kwamba unapoona kitu chochote katika hali ya kawaida, ni mfano wa kitu cha kiroho. Unaona? Vitu vyote vilifanywa kutokana na vitu ambavyo havionekani. Unaona, cha kawaida basi kimeakisi cha kiroho.

24 Sasa, nilipokuwa nikisoma siku chache zilizopita, na ninaamini nililitaja jana usiku, kidogo, kwamba nilikuwa nasoma mahali. . .au kusikia kwenye redio, nikiingia kutoka Canada, ambapo daktari mmoja hapa Marekani alikuwa—alikuwa ametoa kauli kwamba "mwanadamu alikuwa miaka milioni kumi na nne ya mageuzi." Walichimba mfupa huko Italia, mnamo 1800, mahali fulani katika miaka ya 1800, kwamba mfupa huu ulipaswa kuwa mfupa wa binadamu ambao ulikuwa. . .huenda kwa. . .Wakati wanafanya hivyo, kusema ulikuwa na umri gani, naye daktari huyu kama mzee na ameweka maisha yake yote kwenye uchunguzi juu ya mfupa huu. Naye anasema, "Mfupa huu ni mfupa wa mtu ambaye ana umri wa miaka milioni kumi na nne."

25 Sasa, huo ni upuuzi ulioje! Jinsi mtu ameyatupa maisha yake bure, akijaribu kulikanusha Neno la Mungu, naye hana chochote ila tu mwi—mwisho usio na kikomo kutoka kwake. Na mtu yeyote anajua kwamba kama ungezika mfupa ardhini, ndani ya miaka ishirini mfupa huo unageuka. Ndani ya miaka mia moja huo mfupa unakaribia kutoweka, vipande vyake tu, na haidhuru ungeuweka katika hali gani. Unaona? Na kisha ndani ya miaka elfu moja mfupa huo ungekuwa nini, miaka mia kumi? Loo, itakuwa nini mara kumi hiyo, ingekuwa milioni moja? Kisha kumi na nne mara milioni. Loo, jamani! Ni ninii tu. . .Sio busara hata kufikiria kitu kama hicho. Mfupa hautadumu miaka milioni kumi na nne chini ya hali yoyote. Mtu yeyote anajua hilo. Huenda aliokota kitu kilichofanana na mfupa ama kitu fulani.

Na basi wangewezaje kujua ilikuwa na umri wa miaka milioni kumi na nne? Unaona? Isitoshe, Mungu aliumba mwanadamu duniani miaka elfu sita iliyopita, na hilo latosha.

26 Mtu fulani alikuwa akijadiliana nami wakati fulani uliopita, kwenye mmoja wa mikutano yangu. Nilikuwa nikizungumza juu ya mageuzi ya mwanadamu, na nikasema alikuwa na umri wa miaka elfu sita tu. Na mtu huyu akasema, "Vema, Ndugu Branham, tunaweza kuthibitisha ya kwamba ulimwengu una umri wa mamilioni ya miaka. Kwa hivyo kitu unachozungumzia, umekosea kabisa."

Nikasema, "Hivi huamini Biblia?"

Akasema, "Ninaamini kwamba mwanadamu aliandika Biblia."

27 Nami nikasema, "Kweli mkono wa mwanadamu ulitengeneza herufi, lakini Roho Mtakatifu alikuwa nyuma ya mkono huo. Unaona, iliunda herufi, maana Biblia ilisema hivyo."

28 Naye akasema, "Naam, huko—huko, huna budi kukiri kwamba wamekosea duniani."

Nikasema, "Biblia haijakosea, kamwe haikosei."

29 Akasema, "Kweli, ikiwa ulimwengu," kasema, "ilikuwa, unaweza kuona milima jinsi ilivyosukumwa kutoka kwa volkeno."

Nikasema, "Lakini wewe ninii tu . . . "

Akasema, "Na Mungu aliumba ulimwengu huo kwa siku sita."

30 Nikasema, "Sasa, Biblia haikusema hivyo. Ulifikiri tu ilisema." Nikasema, "Hebu turudi sasa kutatua hoja yako. Sura ya kwanza ya Mwanzo, ilisema, 'Hapo mwanzo Mungu aliumba mbingu na nchi.' Nukta! Alikuwa akifanya hivyo kwa muda gani, sijui. Hakutuambia. Lakini, 'Hapo mwanzo Mungu aliumba mbingu na nchi.' Nukta! Kisha, 'Na nchi ilikuwa . . . -tupu.'" Hapo ndipo Mungu alipoanza kuitumia. Unaona? Kwa hiyo wanapiga tu akili zao bure. Unaona? Unaona?

31 Mungu aliumba dunia. Huenda alikuwa amechukua miaka trilioni mia moja kuiumba; sijui alichukua muda gani, lakini aliiumba. Naye hakusema alichukua muda gani, na hautuhusu kuwa ulikuwa ni muda gani. Alisema tu, "Hapo mwanzo Mungu aliumba mbingu na nchi." Nukta! Hiyo inatosha. Hayo ni yote. Alikuwa akifanya hivyo kwa muda gani, hiyo si . . . Lakini basi uumbaji ulianza kuchipuka sasa katika wakati ule mwingine, wakati Yeye alipoanza.

32 Nami naamini, ya kwamba mle ndani, ya kwamba kila kitu duniani kinaakisi Mbingu. Ninaamini hivyo, kwa sababu unaona kila kitu kinang'ang'ania maisha ni kwa sababu kuna maisha ambayo yanaakisiwa kutoka kwake. Nami ninaamini

kwamba Mungu alipomwumba mwanadamu, alianza kuakisi vitu vidogo kama vile uhai wa wanyama, na kisha kitu kingine alichoumba kilikuwa ni kitu tofauti. Hivyo ndivyo hasa Biblia inavyosema Yeye alifanya jambo hilo. Aliumba kwanza miti na uhai wa mimea, na akamwumba mwanadamu. Na halafu kitu cha mwisho kilichopata kutoka duniani katika umbo la uumbaji kilikuwa ni mwanadamu, hakuna kitu cha juu zaidi kilichopata kuja. Kwa sababu nini? Ilikuwa ni mwonekano mkamilifu wa aliye juu zaidi Mbinguni, ambaye, Mungu ni Mwanadamu. Unaona? Mungu ni Mwanadamu, kwa hiyo basi inathibitisha jambo hilo. Na wakati Mungu aliposhuka kukaa kati yetu, Yeye alikuwa Mwanadamu. Unaona? Mwanadamu, kwa hiyo inaonyesha kwamba ukamilifu wa mageuzi ulikuwa ni Mungu, ambaye ni Mwanadamu.

33 Na kisha unachukua mti, (unachukua nyasi na kadhalika), kuchukua mti, unaakisi Mti wa Uzima ulio Mbinguni. Mambo haya yote yanajitahidi kupata ukamilifu. Na kila kitu cha asili, kama Waebrania isemavyo hapa, kilifanywa kwa vitu ambavyo havionekani. Kwa maneno mengine, ni vya kimbinguni. Na kile kisicho cha kawaida kinaakisi kile cha asili. Unaona? Sasa, basi cha kawaida kilikuwa cha Milele, ama kitadumu milele na cha kimbinguni, lakini dhambi ilipotosha cha kawaida. Kwa hivyo, na ikiwa ndivyo, ambayo naamini ndivyo, basi kila kitu kinachotendeka duniani ni mfano wa mambo ya kiroho yanayotendeka. Unaona? Hakina budi kuakisi jambo fulani, mafanikio ya mwanadamu.

34 Sasa, tunaona, kama mwili wa kawaida, huu hapa mwili wa kawaida, na mwili uliumbwa ujizalishe wenyewe, ambao ulikuwa ni watoto. Na sasa mwili wa kawaida, katika kuzaliwa kwa kawaida kwa mtoto, tunaona kitu cha kwanza kinachotokea ni maji, halafu damu, na kisha uhai. Tunaona katika mwili wa kiroho wa Kristo, kitu cha kwanza ni maji, na Damu, na Uzima; kuhesabiwa haki, utakaso, ubatizo wa Roho Mtakatifu. Ona jinsi inavyoakisi, mambo yote ya kimaumbile yakiakisi mambo ya kiroho. Kuzaliwa kwa kawaida.

35 Tunachukua, kwa mfano, ndoa kwa ajili ya mwungano. Tunaona ya kwamba, ndoa; tunapata uchumba, na makubaliano, na kisha ndoa. Hiyo inapaswa kusuluhisha kwa wakati wote. Sasa, hivyo ndivyo ilivyo kwa Kristo na Kanisa. Unaona? Uchumba, Mungu akiita mioyoni mwetu; tunajisalimisha; sherehe ya ndoa, na Bibi-arusi huchukua Jina la Bwana-arusi. Unaona? Unaona? Unaona? Hiyo hapo, hiyo inamfanya Bibi-arusi. Sasa, kila mara bibi arusi huchukua jina la bwana arusi.

36 Kuna mambo mengi sana ambayo tunaweza kuongea hapa. Ninayo orodha iliyoandikwa ambayo ilinichukua saa mbili kuimaliza, karibu, na Maandiko kuunga mkono jambo hili, kama vile ukitaka baadhi yao hapa kuliunga mkono. Kama vile Yohana wa Kwanza 5:7, inavyoonyesha kuzaliwa kwa kawaida

na kiroho, na kadhalika, "maji, Damu na Roho." Na watatu Mbinguni, "Baba, Mwana na Roho Mtakatifu," hawa watatu ni mmoja. Wako watatu wapatanao duniani, si mmoja, bali hupatana kwa habari moja, duniani, hiyo ni "maji, Damu na Roho." Tazama, "maji, Damu na Roho," kama kuzaliwa kwa kawaida kunavyoifananisha.

37 Kwa hivyo ikiwa mtu huweka mawazo ya "kuhesabiwa haki tu ndiyo yote unayopaswa kuwa nayo," amekosea, amekosea. Hana budi kuwa makosani. Na basi ikiwa kanisa linaloamini kama Wapentekoste wengi, kwamba Roho Mtakatifu ndiye, "ni hayo tu, tubu tu na upate Roho Mtakatifu," hilo bado ni kosa, kwa sababu huna budi kupata utakaso mle ndani ili kuitakasa kabla Roho Mtakatifu hajaingia. Usipofanya hivyo, unaiacha Damu. Unaona? Na Kuzaliwa upya, kama vile watu huzungumza ya kwamba ubatizo wa Roho Mtakatifu ni Kuzaliwa upya. Sasa, hilo ni kosa. Ubatizo wa Roho Mtakatifu ni tofauti na Kuzaliwa upya. Kuzaliwa upya ni wakati unazaliwa mara ya pili. Lakini Roho Mtakatifu ni wakati nguvu zinapokuja katika Kuzaliwa huko kwa ajili ya huduma. Hiyo ni kweli. Unaona? Roho Mtakatifu ni . . . kubatizwa katika Roho Mtakatifu.

38 Kuzaliwa upya, una Kuzaliwa upya kwa kumwamini Bwana Yesu Kristo. Unaona? Kwa kuwa na imani na kumkubali kama Mwokozi wako, huko ni Kuzaliwa, unaona, kwa sababu umepita kutoka mautini kuingia Uzimani. Sasa, ukitaka kuunga mkono jambo hilo, chukua Yohana Mtakatifu 5:24, "Yeye ayasikiaye Maneno Yangu na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa milele." Unaona, ana Uzima kwa sababu anaamini. Na kundi lilo hilo ilibidi liende Pentekoste kubatizwa na Roho Mtakatifu. Hasa.

39 Roho Mtakatifu ni nguvu kwa ajili ya huduma. Kwa hiyo tunapozungumza kuhusu wewe huna budi kuzaliwa mara ya pili, na kulitumia hilo kwa Roho Mtakatifu, wengi wa Wamethodisti na kadhalika wamekosea hapo. Haiwezi. Haitaendana na Maandiko hapa. Unalifanya jambo hilo kwenda kombo. Haina budi kulichukua jinsi Maandiko yalivyoliweka hapa. Unaona? Na Roho Mtakatifu ni . . . "Utapokea Kuzaliwa upya baada ya hili"? Nini? Hapana. "Mtapokea nguvu," Matendo 1:8, "baada ya huyu Roho Mtakatifu kuja juu yenu." Unaona? Nao walikuwa tayari wameamini hata Uzima wa Milele, na kadhalika, lakini iliwabidi kuwa na Roho Mtakatifu kwa ajili ya nguvu. "Mtakuwa mashahidi Wangu baada ya Roho Mtakatifu kuwajilia juu yenu," kwa sababu Roho Mtakatifu ni shahidi wa ufufuo, akionyesha kwamba umekuwa mtu mzima katika Kristo.

40 Sasa, ya asili. Mambo yote ya kiroho, matukio yote na kadhalika hugusa, au hufananisha yale ya kimbinguni, au ya—ya asili ni mfano wa ya kimbinguni.

41 Sasa, nilienda kwenye Maonyesho ya Ulimwengu tulipokuwa karibu nayo huko Spokane, na nilifikiri ningeipeleka familia.

42 Kwa sababu nilikuwa kwenye Onyesho moja tu la Ulimwengu huko Marekani, na hapo ni wakati ilipokuwa huko Chicago, miaka iliyopita, mimi na Hope tulienda huko. Na hatukukaa pale ila kama siku moja, wezi wa mifukoni, na kila kitu. Alikuwa na pini ambayo binamu yangu alimpa, nami nikitembea moja kwa moja kando yake, mtu fulani akaiondoa pini hiyo. Ninii. . .ilikuwa inatisha sana. Na hivyo mimi. . . Tulikaa siku moja tukarudi.

43 Lakini Maonyesho ya Ulimwengu, nilichukua familia na kwenda. Haikuwa zaidi ya Maonyesho ya Louisville papa hapa. Umeona Space Needle waliyozungumzia, haikuwa kitu kingine ila nenda hapa kwenye Jengo la Elsby-. . ., au, Jengo la Brown, au mahali fulani, na kwenda juu kama safari nane ama kumi kwenye lifti na kurudi chini. Hiyo tu. Na nadhani hiyo General Electric ndiyo iliyokuwa nayo hapo. Lakini kulikuwa na jambo moja ambalo lilikuwa linajitokeza. Sasa, Ujerumani walikuwa na maonyesho yao, Urusi na mataifa mengine yote walikuwa nayo, kwa sababu ni Maonyesho ya Ulimwengu. Ujerumani, Ufaransa, na maonyesho hayo madogo hayakuwa chumba kikubwa zaidi kuliko vile mimbara hii ingekuwa papa hapa.

44 Lakini wanasayansi walikuwa na mafanikio yao, na jambo kuu walilokuwa—walilokuwa wakifanyia mazoezi, lilikuwa ni matumizi ya tumbaku. Na kama mtu yeyote anayevuta sigara na kuingia mle, na kutoka na kuvuta sigara tena, kuna kitu kibaya na akili ya mtu huyo. Nilipowaona kwa macho yangu wakichukua sigara na kuiweka kwenye mashine, na kuvuta mo—moshi wa tumbaku kutoka hapo na kuivuta kupitia bomba la kemikali, na ile kansa nyeupe ikajaa tu hiyo, kwa sigara moja. Na kisha akasema, "Watu wengi husema," haya duniani kote, mafanikio ya juu zaidi juu yake, kasema, "watu wengi wanasema, 'mimi siivuti ndani.'" Na mwanasayansi akaichukua sigara mwenyewe na kuipulizia kinywani mwake, bila kuipuliza kupitia pua zake, au hata hivyo wanaiteremsha kwenye mapafu yao, lakini akaiweka tu kinywani mwake na kuipuliza kwenye kemikali zilezile, hakukuwa na kansa ndani yake. Akasema, "Ilienda wapi? Katika kinywa changu. Ninapomeza, huenda ndani ya tumbo, bila shaka." Akasema, "Sasa . . . "

45 Kisha wazo likaja, "Kwa nini madaktari wanasema kwamba sigara hazina madhara?"

46 Akasema, "Mtu yeyote ambaye angeuza haki zake za mzaliwa wa kwanza! Daktari akitoa kauli kama hiyo anaweza kustaafu, kwa sababu hizo kampuni za sigara zitampa vya kutosha kustaafu." Hakika anauza haki zake za mzaliwa wa kwanza, maana aliapa kutofanya jambo kama hilo. Lakini wanafanya hivyo kwa vyovyote vile.

47 Naye akasema, "Hii hapa mashine sasa. Tutakuthibitishia hilo kwa mafanikio ya kisayansi." Nao walikuwa na Yul Brynner, mwajua, yule bingwa wa sinema mle ndani. Hiyo, na wakati kile kifurushi kidogo cha nikotini . . . Alisema, "Sasa wanasema 'chujio kwenye ncha.'" Akasema, "Mtu anayefanya hivyo, anaonyesha tu hali yake ya kiakili. Kwa maana kama huna moshi wowote, huna lami, na lami huleta moshi. Na ikiwa unavuta sigara yenye chujio kwenye ncha," kasema, "itahitaji kama tatu au nne ili kukidhi kile ambacho moja ya zile zingine, kwa sababu inahitajika lami zaidi hivyo ili kutosheleza." Usipopata moshi, hakuna lami. Lazima uwe na lami ili kuwa na moshi. Hivyo ndivyo ilivyo. Kasema, "Moshi, ikiwa utaivuta, vuta moja ambayo haina ncha juu yake. Anapata . . . Sigara moja itatosheleza ambapo inahitajika tatu za ile nyingine, maana unavuta tu lami kidogo sana."

48 Ni ujanja wa mauzo! Hayo tu ndiyo taifa limejaa ni ujanja wa mauzo, na uchafu na chochote kile.

49 Na hapo ndipo akaichukua hiyo na kuonyesha jinsi hicho kifurushi kidogo kilinaswa kooni ama kwenye mapafu. Na kwanza ni nyeupe, kisha inageuka waridi, na kisha kutoka waridi inageuka zambarau. Chembe—chembe ya seli ndogo ilionekana kuwa kubwa *hivi* kupitia kioo, lakini, bila shaka, unachukua kioo chenye nguvu hata kuona seli. Kisha anasema, "Inapogeuka zambarau, una kansa." Akasema, "Mtu ambaye atavuta pakiti moja ya sigara kwa siku ana uwezekano wa asilimia sabini kufa kwa kansa kuliko mtu asiyeivuta." Na inaonekana ni ujinga kujihatarisha hivyo.

50 Sasa, halafu akachukua jambo lingine na kulithibitisha, akatoa panya mweupe. Naye akachukua sigara na kuiweka kwenye mashine, na kuivuta juu ya kitu fulani kama marumaru nyeupe, na kuchukua u—usufi, na kuchukua nikotini iliyotoka kwa sigara moja na kuipaka kwenye mgongo wa panya. Kila baada ya siku saba walikuwa na panya mwingine akitoka. Na wangelazimika kuwa na kila mmoja kwa ajili ya somo la siku hiyo. Na kumweka panya huyo ndani kwa siku saba na kumtoa nje, kansa ilisimama juu *hivi* kwenye mgongo wa huyo panya. Baadhi yao hawaishi hata kumaliza hizo siku saba. Huyo panya asingeweza kusonga. Sikuweza kula kwa siku mbili au tatu, kutazama hicho kitu kibaya, akiwa amesimama pale akiwa na hiyo kansa, nayo inashuka juu ya miguu yake na kadhalika namna hiyo, kansa ndefu kubwa ilivimba karibu nusu inchi mgongoni mwa huyo panya, nikotini kutoka kwa sigara moja. Na unafikiri hiyo iliwazuia? Jamaa mkubwa aliyeketi karibu nami pale, na jasho likatiririka usoni mwake, akasema, "Kidogo inashangaza, sivyo?"

Nikasema, "Je, wewe huvuta sigara?"

Akasema, "Naam, bwana, mimi huvuta."

51 Nikasema, "Vema, basi unapaswa kuacha hilo." Lakini ndivyo hivyo, mafanikio, kile wanachoweza kuthibitisha kwamba kinafanya hivyo.

52 Sasa, nilibashiri kwamba ulimwengu unasimama na kama ustaarabu upo, zamani wakati wa marufuku wakati kulikuwa na faini kubwa sana kuuza chupa ya wiski, itakuwa mara kumi ya faini hiyo kuuza pakiti ya sigara katika miaka michache kutoka sasa, kama ustaarabu upo. Ni mbaya mara kumi kuliko wiski. Hakika ni mbaya. Ni—ni mwuaji, hiyo. Na unaweza kuwaambia watu kuihusu, na hawalitilii maanani hata kidogo. "Ni mhubiri mtakatifu anayejibiringisha," na kuiacha. Unaona, ndivyo hivyo, hawatambui.

53 Lakini, hoja yangu ni hii, ni mambo gani ya kisayansi yameweza kufanikisha. Walikuwepo kwenye Maonyesho ya Dunia, wakionyesha kwa utafiti wa kisayansi kile sayansi imeweza kufanikisha katika mambo ya asili. Sasa, tuko hapa tukionyesha kwa utafiti wa kiroho kile ambacho Mungu ameweza kufanikisha kwa watu ambao wataliamini Neno Lake. Sasa, ili kufanikisha mambo ya kisayansi, lazima ufanye kazi katika mistari ya kisayansi. Ili kufanikisha mambo ya kiroho, huna budi kufanya kazi katika mistari ya kiroho. Sasa, unafikiri panya huyo alionekana wa kutisha, ambapo alionekana, ungepaswa kumwona! Laiti ningekuwa na picha yake, hata, ya kuonyesha. Kama ningeipata, ningeipata, lakini hawangekuruhusu kuichukua. Lakini angalia. Bila shaka, huyo panya anaishi kwa saa chache tu zaidi, baadhi yao hawaishi hata wakamaliza siku saba. Lakini wazia hilo!

54 Unafikiri huyo alionekana ameoza, unapaswa kuona jinsi nafsi inavyoonekana ambayo imeikataa Injili. Unapaswa kuona jinsi zinavyoonekana za kutisha. Jinsi ibilisi anavyomshika mtu na anaweza kumpotosha mwana wa Mungu kuwa kitu cha kuchukiza, kama vile alivyo machoni pa Mungu. Loo, anaweza kuwa na urefu wa futi sita, na mabega kama sijui nini, na nywele zilizojisokota na *nini*, hiyo haimaanishi chochote. Ni ndani ya mwanadamu ndio unadumu. Nje ni vumbi, hata hivyo.

55 Kwa hivyo ni mafanikio, na kisha wangeonyesha, walikuwa na sindano hii ya nafasi na kila kitu, kile walionyesha kufanikisha, yale waliyokuwa wameweza kufanya, na kueleza atomiki zao zote na kadhalika. Walikuwa na utabiri wa kile Chevrolet ingekuwa. General Motors walikuwa nayo kwenye onyesho, kile ninii . . . katika nyingine, karne inayofuata, Chevrolet ya karne ya ishirini ingeonekanaje. Ilionekana kwangu kama bo—bomba la gesi na kofia juu yake. Sasa, walionyesha jinsi ingefanya kazi na ingewaka kwa nguvu za atomiki na aina fulani ya bawa ambalo linaweza kuinuka juu ya mtu mwingine na kudhibiti. Hiyo ingekuwa fa—faida kubwa.

56 Lakini sijui kama tungeweza kurejea katika kurasa za Kitabu cha Mungu, asubuhi ya leo, na kuona jinsi kanisa

litakavyoonekana wakati huo, tuone mafanikio ambayo Mungu amefanya. Loo, jinsi ambavyo matukio daima katika dunia hii yanawakilisha kitu kinachotoka mahali pengine; lakini inapoipiga dunia, kwa kawaida iko katika hali potovu kwa sababu iko katika ulimwengu wa giza na dhambi. Unaona? Lakini basi kuna uwakilishi wa kweli katika nyanja za kiroho za mwelekeo mwingine. Kutoka kuwa katika viwango vitatu, basi kiwango cha sita kina uwakilishi wake. Nimefurahia sana hilo.

57 Sasa, hebu tuchukue tu mafanikio ambayo tumeweza kufanya katika miaka michache iliyopita. Sasa, hebu tuanzie kwenye jambo ambalo limetokea. Sitawaweka muda mrefu, Bwana akipenda, lakini nataka muone hili haraka. Na, loo, iliponijia, nilijisikia kuruka niende. Sasa angalia, sasa, miaka michache iliyopita usafiri ulikuwa wa farasi na mkokoteni, si muda mrefu sana uliopita, zamani sana. Nilizunguka kote katika farasi na mkokoteni, na juu ya tandiko. Nilipokuwa mvulana, umri wa miaka kumi na mitano, kumi na sita, nilipanda farasi, na nilikwenda mjini kwa farasi na mkokoteni, nikiendesha moja kwa moja karibu na kanisa hili hapa, barabara yenye matope huko nje, na kinamasi hapa kilichojaa magugu marefu kama jengo, karibu, ya farasi na mkokoteni, kutoa maharagwe manjano na kadhalika kutoka shambani.

58 Sasa ninaipita kwenye gari la mafuta na gesi. Ni tofauti iliyoje! Siku ya farasi na mkokoteni, kisha siku ya motokaa.

59 Na ndipo siku ya ndege ikaja, iliyotoka duniani kwenda angani. Sasa, kama utaangalia, kwa hakika kama mafanikio hayo yalivyokuwa kwa sayansi, ikiwa mtu huyo atakuwa na akili ya kiroho na kuelewa, iliwakilisha mafanikio ya uchumi wa Mungu na Kanisa Lake. Sasa siku . . .

60 Na, kumbukeni, mjumbe daima huja mwishoni mwa Ujumbe. Tunajua katika nyakati za kanisa pale jinsi tulivyopata jambo hilo.

61 Sasa, siku za farasi na mkokoteni alikuwa nani? Huo ulikuwa mwisho wa wakati wa Kilutheri. Unaona, siku za farasi na mkokoteni. Waliamini katika kuhesabiwa haki. Mungu akilileta Kanisa kutoka kwa Urumi, Ukatoliki, akalileta katika mafanikio yake ya kwanza ya kiroho, kwamba, "Mwenye haki ataishi kwa imani." Hiyo ilikuwa siku za farasi na mkokoteni, walipokuwa wakitoka . . . kwa siku za farasi na mkokoteni, hiyo iliisha.

62 Sasa, mafanikio yaliyofuata ambayo mwanadamu alikuwa nayo katika njia ya usafiri yalikuwa ni motokaa. Na, unaona, hiyo motokaa huongezeka kila wakati, katika nguvu zake.

63 Sasa, mwishoni mwa wakati wa Wesley, ulioletwa na mafanikio ya kiroho, utakaso, ambayo inamaanisha kanisa lililoinuliwa kutoka katika hali ya kuhesabiwa haki hadi hali ya kutakaswa.

64 Sasa, ninawatakeni mkumbuke jambo hili tunapoendelea, kwamba kanisa linaloitwa "kanisa" si Kanisa. Kanisa ni Kanisa, la kiroho! Makumi ya maelfu mara maelfu ya Walutheri waliojiunga na kanisa, hawakujua zaidi juu ya kuhesabiwa haki kuliko nguruwe alivyojua juu ya tandiko la pembeni. Wao—hawakujua lolote juu yake. Na katika wakati wa Wesley, jinsi makumi ya maelfu walivyokiri utakaso, hawakujua zaidi juu ya nguvu za Mungu za kutakasa kuliko—kuliko sungura anavyojua kuhusu viatu vya theluji. Unaona, hawakujua kabisa.

65 Lakini kulikuwa na watu ambao walilifanikisha. Haleluya! Mnaona ninapofikia. Kulikuwa na mtu aliyejua kile "kuhesabiwa haki" kulimaanisha mbele za Mungu, "tukiwa na amani na Mungu kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo." Kulikuwa na baadhi ya hao Walutheri waliokuwa waaminifu. Waliamini Hilo. Haidhuru kanisa Katoliki lilisema nini, waliamini Neno la Mungu na kusimama juu Yake kwa sababu mjumbe wa wakati huo alihubiri "mwenye haki ataishi kwa imani," na wakaamini katika hali ya haki. Nao waliweza kwa neema ya Mungu kupata kuhesabiwa haki, kuwa na amani na Mungu kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo.

66 Sasa, tunaona tena, wakaja Wamethodisti wakiwa na utakaso. Kulikuwa na wengi wa wale Wamethodisti ambao kwa kweli walikuwa wametakaswa. Sasa, kuna wengi wao walidai hilo na hawajui lolote kulihusu. Kanisa la Methodisti lilifundisha utakaso. Walisema walishuka na kulia na kuinuka tena, wakasema, "Utukufu kwa Mungu, nimetakaswa!" Nao wakaendelea kuishi moja kwa moja kama walivyoishi siku zote. Lakini baadhi ya wanaume na wanawake hao walikuwa wametakaswa kutoka katika mambo ya ulimwengu, na kuishi maisha yaliyotengwa, yakawekwa wakfu. Kwa nini? Huo ulikuwa ni wakati wa motokaa ambayo ilichukua nguvu zaidi ya farasi. Motokaa, mtindo wa zamani wa T labda ulikuwa na nguvu za farasi kumi na watano au ishirini. Unaona, walikuwa na farasi kumi na watano ama ishirini waliowekwa kwenye chupa ndogo namna hiyo. Utakaso! Wakati sayansi ilipofanikisha kitu kwa—kwa—kwa hali ya kawaida, Mungu anafanikisha jambo fulani kwa njia ya kiroho. Unaona, jambo fulani linaendelea kila wakati. Na kisha baada ya wakati uliotakaswa . . .

67 Sasa, tunamchukua mtu kama mzee Bevington. Jamani, ni nani angekuwa mtu mkuu kuliko Ndugu mzee Bevington? Basi mtazame John Wesley, George Whitefield, Finney, Knox, wengi wa wale Wamethodisti wa kale waliotoa jasho. Walipitia kuzimu duniani, mateso, kwa sababu waliamini kwamba Neno la Mungu lilifundisha utakaso, hatua ya pili ya neema, nao wakadumu nayo, nao wakaiamini, na wakafanya maajabu nayo. Sawa tu na Henry Ford na hao wengine walivyofanya na usafirishaji wa T Ford-muundo wa zamani kando na farasi, aliendelea na

kupita siku ya farasi. Naye Wesley alisonga mbele kupita siku ya Kilutheri.

68 Na kisha ikaja Pentekoste. Na kama sayansi ya ulimwengu iliweza kufikia i—injini ya motokaa, Wright Brothers ambao waliunda au kutengeneza, kutengeneza, hasa, ndege, mashine ya kuruka ilikuwa mbali sana kuliko motokaa duniani, kwa sababu alipaa hewani. Sasa, Wright Brothers, kupitia mafanikio yao, waliweza kuchukua sayansi na kuiga kitu hapa duniani, kuonyesha ya kwamba kulikuwa na jambo kuu la kiroho lililokuwa karibu kutukia. Na wakati Wright Brothers waliweza kufanikiwa kufanya miguu ya mtu kutoka ardhini, Pentekoste ilishuka na kupaa hewani kwa karama ya kiroho, pamoja na ubatizo wa Roho Mtakatifu. Aliingia hewani! Loo, haleluya! Aliondoa miguu yake ardhini ili aweze—aweze kuogelea huku na huko, akapaa juu angani! Loo, jinsi alivyokuwa juu zaidi ya farasi na mkokoteni! Jinsi alivyokuwa mbali zaidi ya motokaa! Alikuwa juu angani. Alikuwa akigonga na kupuliza na kugonga, lakini alikuwa akiruka. Unaona, yale ambayo mwanadamu anafanikisha duniani, kwa maana yamefanywa kwa vitu ambavyo havionekani. Mungu aliweza kupata kitu kupitia watu waliojazwa na Roho waliokuwa na njaa na kiu, na wale ambao wangedumu na Neno.

69 Sasa, kama Wesley hangalijitokeza kwenye Neno na kupata jina baya nyuma yake, aliitwa mtu mwenye kichaa, na kila kitu kingine, hangeweza kufanikiwa. Lakini Wesley alikuwa mmoja wa wanasayansi wakuu wa Mungu. Luther alikuwa mmoja wa wanasayansi wakuu wa Mungu. Hawakujali yale makanisa yalisema, yale madhehebu yalisema. Luther hakujali yale Wakatoliki walisema, aliamini wenye haki wataishi kwa imani! Haleluya! Naye alichukua kemikali za Mungu za Neno na kuziweka pamoja, na kanisa likatembea kwa imani. Wesley aliliunganisha kwa Damu, na kulithibitisha kwa Damu, nalo kanisa likatakaswa. Wapentekoste waliamini kwamba ubatizo wa Roho Mtakatifu, kwamba ahadi ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa wale walio mbali, nao wakaweka pamoja kemikali kutoka kwenye Neno, nao wakaingia hewani. Haleluya! Walihama, kwa sababu waliweza kuwa na uwezo wa kukamilisha hayo.

70 Sasa, kwa nini watu hawa wakafanya hivi? Kwa nini Luther akaipata? Kwa nini Wesley akaipata? Kwa nini hawa wengine? Kwa sababu nyenzo zilikuwa zimewekwa hapa duniani ambazo zingeweza kutengeneza Ford muundo wa-T. Kulikuwa na umeme ambao ungeweza kufanya mo—motokaa kukimbia. Kulikuwa na petroli duniani, kulikuwa na pistoni na kadhalika, mitambo yote, kaboni ya jenereta, na kila kitu walichopaswa kuwa nacho ili kuunda kitu hiki, na angalia kilianza. . .kuitengeneza, hasa, sio kuiumba. Mungu ndiye Muumba, alikuwa nayo hapa. Lakini mwanadamu ambaye

aliamini katika ulimwengu wa kisayansi, wa asili, alichunguza ndani yake, na hawangekubali “hapana” kuwa jibu. Waliamini. Ulikuwa ni ufunuo moyoni mwao, nao walidumu nao mpaka walipothibitisha kwamba ni kweli.

71 Hivyo ndivyo ambavyo John Wesley alithibitisha utakaso. Nye—nyenzo hizo zilikuwa zimewekwa hapa, Neno la Mungu lililoileta. Aliliamini! Haidhuru kama kanisa zima, kanisa la Anglikana na wote walimkataa, alidumu na imani yake na akaithibitisha. Na Wapentekoste wakaja na kuthibitisha, kwa sababu walikuwa na nyenzo, kwamba Roho Mtakatifu alikuwa sahihi. Na wakapaa angani.

72 Je, uliona, moja—moja ya mafanikio hayo ya kisayansi yalifuatana na yale mengine, yalikamilisha yale mengine. Ilikuwa tu ni hali ya juu zaidi. Unaona? Motokaa ilikuwa usafiri wa hali ya juu kuliko farasi, na ndege ilikuwa usafiri wa hali ya juu kuliko motokaa, lakini zilienda pamoja. Nguvu za farasi! Amina! Ikiwa hiyo ni nguvu ya farasi, vipi kuhusu nguvu za Mungu? Vipi kuhusu Roho Mtakatifu na nguvu? Nguvu za Roho Mtakatifu zinazoweza kukuhesabia haki, nguvu zile zile za Roho Mtakatifu zinaweza kukutakasa. Nguvu zile zile za Roho Mtakatifu zinazokutakasa, zinaweza kukujaza na Uwepo Wake. Na maskini sayansi, ambayo haikujua ABC zao, iliipata. Kwa nini? Walikuwa wanasayansi wa kiroho. Amina. Waliona jambo hilo, wakaliamini. Mwanadamu alifanya hivyo kwa elimu, mwanasayansi wa asili. Mwanasayansi wa kiroho alifanya jambo hilo kwa ufunuo. Moja kwa elimu, nyingine kwa ufunuo. Loo, kama tunaweza tu kufungua. Kuna kila aina ya nyenzo zimewekwa hapa. Hiyo ni kweli.

73 Sasa tunaona jinsi inavyoenenda, jinsi Mungu alivyoweza kufanikisha jambo hilo. Katika Wapentekoste, wakapaa angani. Jinsi wao . . . Ndipo ikarudishwa kwa kanisa, uponyaji, kunena kwa lugha, ufunuo, karama za Roho. Hilo, Luther hakujua lolote kulihusu, wala Wesley hakujua. Hawakuwahi kulifundisha, hawakujua lolote kulihusu. Ilikuwa nje ya wakati wao.

74 Mbona, Henry Ford angejua nini kuhusu ndege siku hizo kabla ya Wright Brothers? Unaona, hawangelijua. Kisha kitu kile kile ambacho m—mtu kule nyuma na kuendesha farasi na mkokoteni, miaka mia tano iliyopita, asingejua lolote kuhusu gari lisilo na farasi, ni Biblia tu ilisema lingekuwapo. Kwa hiyo waliweza kuifanikisha kwa utafiti wa kisayansi. Na ilipotukia duniani, Mungu aliiwakilisha kwa mafanikio kwa Kanisa Lake. “Kwa maana vitu vilivyopo, vinavyoonekana, viliumbwa kwa vitu visivyoonekana.” Unaona, uakisi wake.

75 Sasa, sasa wakati wa Kipentekoste, kwa miaka hamsini iliyopita, ametuma uamsho kote ulimwenguni, pamoja na kila aina ya kila kitu ndani yake. Nao wamekuwa na uponyaji, na magonjwa yakiponywa, viwete wakiponywa, vipofu walirejeshewa kuona kwao. Unafikiri ulimwengu

uliamini hilo? Hapana, bwana. Hawakumwamini Luther. Hawakumwamini Wesley. Hawakuwaamini Wapentekoste. Lakini Mungu alichukua Biblia, katika utafiti wake, mtu ambaye alikuwa tayari kufanya jambo hilo, alichukua Biblia na kuithibitishia ya kwamba ilikuwa sahihi. Amina. Sasa hatuna budi kukumbuka jambo hilo, hatuna budi kuliamini, tukiona mambo hayo yalikuwa ni mfano. Sasa tumeishi kwenye wakati wa Kipentekoste. Wakati wa Kipentekoste, kama nilivyothibitisha kule, unaingia katika wakati wa Laodikia.

76 Lakini sasa jambo lingine limetokea. Tuna mwanaanga sasa. John Glenn alikuwa mwanaanga wetu wa kwanza. Nasi tunaona ya kwamba hiyo ni mbali sana kuliko ndege, ndege inaweza tu kwenda hadi kufikia shinikizo lake na kadhalika. Lakini hii ni kwa nguvu za atomiki, nguvu kubwa inayomsukuma juu sana kuliko ndege, ndege hata—hata haiko ndani yake. Hiyo ni kweli. Ameweza kufanya hivyo. Vema. Sasa tuna mwanaanga, enzi ya kawaida.

77 Basi, kumbuka, mjumbe anakuja mwishoni mwa ujumbe uliotangulia, daima. Tumethibitisha hilo hapo. Sasa tuko kwenye mstari wa mwanaanga. Amina na amina! Mungu ame. . .

78 Sayansi imeweza kuthibitisha kuwa kuna mwanaanga ambaye anaweza kwenda mbali zaidi mpaka usingeweza kuiona kwa macho yako ya kawaida, na inaweza kwenda kama kuna shinikizo lolote kule au hakuna. Anaweza tu kwenda huko kwa sababu katika tangi iliyotiwa presha, na anaweza kwenda huko na kuzunguka na kuona ulimwengu wote. Mwanaanga! Loo, jamani, ni wakati wa jinsi gani ambao huo unakuja. Naam, bwana, kupita mambo yoyote ya asili kabisa, na kuingia moja kwa moja huko.

79 Je, inawakilisha nini? Wakati wa kiroho, wakati wa kiroho ambapo Mungu atakuwa na wanaanga wa kiroho. Amina! Wako hapa sasa hivi! Haleluya! Tai wa angani wanaoweza kupita ndege yeyote mwingine, husafiri juu kuliko kila kitu, wanaanga wa kiroho (Utukufu!) wanaoweza kuchukua Neno la Mungu na kuthibitisha ya kwamba Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele. Mwanaanga wa kiroho! Loo, jamani! Utukufu! Hilo linanifanya nijisikie vizuri, kuishi katika wakati huu! Sasa ni jambo la ajabu jinsi gani kwa mwanaanga wa kiroho! Unaona? Ni nini? Wanasayansi wa asili walifanya nini? Wameweza kufikia hilo. Na Mungu, kupitia kwa mwanadamu ambaye angedumu na Biblia na kusema kwamba "Ni yeye yule jana, leo, na hata milele," na asiogope ahadi bila kujali mtu yeyote alisema nini, adumu nayo. Ni nini? Unakuwa katika mwanaanga ambaye anaweza kwenda mbali zaidi ni mbali zaidi ya mawazo ya kimadhehebu. Ni mbali zaidi ya kitu kingine chochote. Ni mbali zaidi ya mambo ya kanisa. Huko mbali pamoja na Mungu na unabaki na Yeye pekee. Wanaanga!

80 Na, kumbuka, ili kuwa mwanaanga, iliwabidi waingie kwenye tangi, nao hawawezi kujidhibiti wenyewe. Inahitaji nguvu za rada, nguvu za atomiki kumwinua huko kupita anga, na kisha anadhibitiwa na mnara. Utukufu! Wanaanga wa kiroho wa Mungu ni vile vile! Wanaingia kwenye tangi, na mahali fulani, ndani ya mwili, na mwili huo ni Mwili wa Kristo. Kisha, sio wao, si—sivyo, haikuwa John Glenn, ilikuwa—ilikuwa ni tangi aliyokuwa ndani yake. Ilikuwa mashine. Aliketi tu pale, hakufanya lolote. Alikuwa tu na ujasiri halisi wa kuamka pale na kusema “ni sawa,” kwa sababu sayansi ilikuwa imethibitisha hilo.

81 Mungu anataka mwanadamu anayeweza kuja ndani ya Kristo na kuamini ya kwamba ni yeye yule jana, leo, na hata milele, na wasichukue mawazo yao wenyewe, waingie angani, wakiongozwa na Roho Mtakatifu. Amina. Wanaanga! Whiu! Ni umbali gani kutoka kwa maskini farasi na mkokoteni! Ni umbali gani hata kutoka kwa ndege! Jinsi ilivyo mbali na kuhesabiwa haki, kutakaswa, ubatizo wa Roho Mtakatifu! Wanafikia tai. Wa kwanza, walikuwa mijusi, kisha wakawa kuku, kisha wakawa kunguru, lakini sasa wao ni tai. Hakuna anayeweza kuwafuata!

82 Tai ni ndege maalum. Anaweza kwenda juu zaidi kuliko ndege mwingine yeyote. Ameandaliwa kuona, kuweka kichwa chake sawa atakapofika huko. Kuna watu wanaweza kuruka juu na hawajui walipo baada ya kufika huko, kwa sababu hawezi kuona mbali zaidi ya kile alichoruka. Lakini kuna wengine ambao wanaweza kuangalia nyuma na kuona kinachoendelea. Huyo ndiye tai. Anaweza kusimama pale mpaka aliangalie, na kungoja mpaka asikie ujumbe unaomwambia la kusema. Huyo ni mwanaanga wa Mungu. Unaona? Imefuata mafanikio mengine yote, kwa nini isifuate mafanikio haya?

83 Wanaanga wa Yesu. Amina. Hata haondoki kwa uwezo wake mwenyewe. Anatiwa nguvu. Kitu pekee anachofanya ni kuingia ndani yake. Hayo tu ndiyo unayopaswa kufanya, ni kuingia ndani yake, Mungu atakutia nguvu na kukuweka mahali pafaapo. Si nguvu za petroli tena, wala, kanuni fulani za imani za kanisa. Ni nguvu za atomu za Mungu zinazokusukuma kabisa huko mbali angani. Amina. Loo! Kwa nini, ni kitu gani, wanaanga hawa? Wamepata . . . Kamwe hawahitaji . . . alichukua tu neno kuhesabiwa haki, neno utakaso tu, ameingia kwenye Biblia nzima. Amina. Ameingia katika hiyo yote, kwa sababu anajua ya kwamba Mungu anaweza kutekeleza kila ahadi aliyowahi kutoa. Anakaa tu hapo na kungojea. Loo, jamani! Neno halina budi kujidhihirisha Lenyewe. Kama wewe ni mgonjwa, na mwanaanga, kumbuka tu, ingia ndani ya Kristo, subiri kuhesabu kinyumenyume. Ni hayo tu. Atafyatua risasi, usijali. Sasa, tumeweza kulifikia kwa sababu Mungu aliliahidi.

84 Sasa, mwanaanga ni mkuu zaidi kiasi gani, mambo haya sasa, kutoka kwa nguvu za farasi wa zamani, nguvu za motokaa,

na—na nguvu za ndege! Unaona, mwanaanga, yuko juu sana hivi kwamba anaweza kuona vitu ambavyo mtu aliye kwenye farasi na mkokoteni hangeweza kuona. Yuko juu sana anaweza kuona vitu ambavyo mtu kwenye motokaa hangeweza kuona. Yuko juu sana hivi kwamba anaweza kuona vitu ambavyo mtu anayeendesha ndege hawezi kuona. Amekwisha kwenda nje ya hoja. Amina. Utukufu! Ndivyo ilivyo. Amekwisha kupita zaidi ya mafanikio yoyote ambayo mwanadamu angeweza kufikiria, shirika, madhehebu, "Huna budi kuwa Mmethodisti, Mbaptisti, ama mfuasi wa *hili*, umoja, uwili," au chochote kile. Yeye ni mwanaanga, amesafiri akaingia angani. Amina. Jinsi nilivyo na shukrani!

85 Na, kumbuka, mwanaanga anadhibitiwa na nguvu za rada. Uliwaona wakimwingiza John Glenn. Nilitazama chini kule Cape Canaveral na nikaona kitu hicho kikubwa cha rada, na hata usingeweza kumwona popote, lakini ungeweza kujua alipokuwa kwa jinsi rada hiyo ilivyokuwa ikielekeza. Hapo ndipo alipokuwa. Unaona? Nasi tuna rada, pia, maombi. Maombi ndiyo nguvu za rada zinazomwongoza mwanaanga. "Mwombeni Baba lolote katika Jina Langu, nitalifanya." Unaona? Angalia tu jinsi maombi yanavyoenda, unaweza kuona jinsi anavyoelekeza. Amina. Angalia tu jinsi kanisa linavyoomba, unaweza kuona jinsi makombora yatakavyoruka. Unaweza kujua kutokana na ji—jinsi wanaanga wanavyosafiri, kutokana na jinsi kanisa linavyoomba.

86 Anaomba, "Bwana, bila shaka hatuamini katika mambo haya." Lo-loo! Mwanaanga huyo anashuka. Ni hayo tu. Loo, ndugu!

87 Lakini wakati yote yanawezekana, "Bwana, mimina Roho Wako juu ya kanisa na ulipe kile tunachohitaji. Tumiminie Roho Mtakatifu, na ututoe tu katika kila hoja, na kuamini ya kwamba Neno hilo ni sahihi nasi tutasimama Nalo." Tazama skrini kisha uanze kuinua kichwa chake namna hii, unaona. Mwanaanga anaendelea na kuendelea na kuendelea, juu kabisa angani. Hum! Ajabu! Anaenda zaidi ya madhehebu yoyote, huenda zaidi ya kanuni yoyote ya imani.

88 Sasa kumbuka, kuhesabiwa haki kumegawanywa kwa kanuni ya imani, hiyo ni kweli, unaamini kuhesabiwa haki kama mahali fulani kama Walutheri na satelaiti zao zozote. Hivyo ndivyo walivyo, satelaiti, lakini hawajatoka ardhini bado. Unachukua utakaso na satelaiti zao. Unasema, "Je, satelaiti kwa Walutheri ni nini?" Vema, Church of Christ na kundi hilo pale. "Je, satelaiti kwa akina Wesley ni nini, kwa Wamethodisti namna hiyo?" Nazarayo, Pilgrim Holiness, satelaiti zao. Halafu Wapentekoste na satelaiti zao, ndege, hakika, umoja, uwili, utatu, unne, haya yote kuendelea, Foursquare, Church of God, yote yangali yana imani katika madhehebu.

89 Lakini mwanaanga huvunja kizuizi cha sauti. Anaendelea kupita moja kwa moja. Hasikii chochote. Loo, jamani! Yeye hupita tu hayo yote. Unaona, yuko juu sana mle ndani ambapo mambo yote . . . Anaishi katika Uwepo wa Mungu. Naam, bwana. Aliahidi jambo hilo, Neno Lake linasema ya kwamba Yeye ni Kuhani Mkuu. Unaona hiyo rada kubwa iliyowekwa pale nje ikisonga? Mwangalie katika mkutano. Unaweza kutazama wakati Roho Mtakatifu anashuka katika umbo la Nguzo ya Moto kama alivyoahidi. Mtu hataketi pale akijaribu kulijadili Hilo na sayansi, mwaminio halisi. Yeye ni nini? Yeye ni Skrini ya Rada. Mwangalie Yeye. Anaanza kuelekeza pande zote. Amina. Nayo inamshika yule pale, yule mwanaanga. "Una kansa. Una *hiki-na-hiki*. Wewe ni *Fulani* kutoka mahali fulani. Bwana Yesu akuponya." Haleluya! Anaondoka. Wanaanga! Loo, jamani, linapaswa kuwa Kanisa la jinsi gani! Iko hapa.

90 Mafanikio hayo yamethibitishwa na sayansi. Waliyaonyesha huko nje kwenye Maonyesho ya Ulimwengu. Tumeyapata. Amina. Yanathibitishwa kila mahali, enzi ya mwanaanga tunayoishi. Tazama, "Ilifanywa kwa vitu ambavyo havionekani." Unaona, ilitengenezwa na kitu fulani kutoka Mbinguni. Ni Mungu Mwenyewe; uko katika kiwango hicho cha sita. Ni uweza wa Mungu. Tumekuwa mahali ambapo hata tumeinuliwa katika hali hiyo, zaidi ya jambo hili la kwenda kaburini na kulia, jambo hili la kuweka nguo ya mfiwa kwenye kipete cha mlango na kusema kwaheri milele. Haleluya! Tayari tumeingia kwa mwanaanga, na tukasafiri kuelekea kule na kuona mahali ilipo, na tukarudi. Utukufu! Tunaenda Nyumbani kupita anga huko ng'ambo, kupita mawazo ya mwanadamu. Jinsi wazee watakavyobadilishwa katika muda wa kufumba na kufumbua jicho. Tutawaona huko, wazee na wanawake, vijana tena. "Unajuaje?" Biblia inafundisha hivyo! Na, Mungu alimwingiza mwanaanga mle ndani, tunajua inahusu nini, akarudi. Hakuna wasiwasi juu ya kufa. Kufa si kitu. Hakika, ni kuishi. Naam, bwana. Ni kuondoa tu miguu yako chini ili tuweze kwenda. Loo, jinsi ilivyo ya ajabu!

91 Ameahidi mambo haya yote katika Neno Lake, kwa kuwa Waebrania 13:8 ilisema, "Ni yeye yule jana, leo, na hata milele." Mambo ambayo aliweza, Mungu angeweza kufanikisha kwa mtu mmoja ambaye angejisalimisha kwake, kwa Neno la Mungu, kwa sababu, kama nilivyosema jana usiku, yeye daima alisimama na Neno.

92 Sasa, unajua nini, wanaanga kwa kweli si jambo jipya. Vipi kuhusu Eliya? Kama hakuwa mwanaanga, sijawahi kuona mmoja. Alikwenda ambapo John Glenn hakuwahi kufikiria kwenda.

93 Vema, unajua, mmoja aliondoka kwa mwendo wa polepole wakati mmoja. Jina lake lilikuwa Henoko. Alipanda tu akitembea, lakini alikuwa mwanaanga. Hakika. Alitiwa presha,

haikumlazimu kubadilishwa, hakuna kitu. Hapana, tayari alikuwa ametiwa presha alipoanza kutembea. Alitembea tu kutoka katika awamu zote na kila kitu, akatembea akaingia katika Uwepo wa Mungu.

94 Na hivyo mzee mmoja alikuwa amechoka na hakuweza kutembea vizuri sana tena. Alikuwa amezozana na Yezebeli, na nywele zake fupi na rangi na kila kitu, mpaka Mungu akateremsha tu gari la farasi, akasema, "Nitakuruhusu tu upande kupitia mawingu alasiri ya leo." Mwanaanga!

95 Wakati mmoja Mmoja alikuja kufa kwa ajili yetu sisi wengine, na Mungu alimfufua katika siku ya tatu. Na watu mia tano wakasimama pale wakamwona akichukuliwa juu mawinguni, huku Sauti ikisema, "Nitakuja tena." Na Malaika wakarudi na kusema, "Yesu huyu huyu aliyetwaliwa juu, Mwanaanga Mkuu, atarudi tena katika njia ile ile, katika namna ile ile ya ghorofa ambayo Yeye yuko, mwili, usioweza kufa." Haleluya! "Nasi tutakuwa na mwili kama mwili Wake Mwenyewe wenye utukufu, kwa maana tutamwona jinsi alivyo." Loo, haleluya! Alipasua vizuizi vyote vya sauti, vizuizi vyote vya hoja, na kwenda mbali kupita hoja, akaenda zaidi ya kitu kingine chochote.

96 Na mtu yeyote atakayeishi kwa ajili ya Mungu itabidi apite hisi zozote tano, itamlazimu kuendea elimu yoyote, mafanikio yoyote ambayo mwanadamu ameweza kupata, na kumwamini Mungu, apasue kila kitu na kukiweka kando, na kupenya kuingia Mbinguni. Amina. Loo, ni wanaanga gani na kadhalika wamepatikana katika hali ya asili, Mungu ameweza kufanya jambo hilo kwa kanisa Lake, kwa watu wa kiroho, kwa watu wa kiroho ambao wataamini. Mwanamume ama mwanamke yeyote atakayethubutu wakati wowote, wakati wowote kumchukua Mungu katika Neno Lake, ni mwanaanga.

97 Watasema, "Loo, hiyo si busara. Unasikia watu hao wakilia, wakipiga kelele, unasikia hili? Loo, hiyo siyo busara hata kidogo." Hiyo haieleweki.

98 Mtu fulani aliniambia, akasema, "Ulikuwa na ndoto, Ndugu Branham, ulipoona mahali hapo." Sikuwa na ndoto. Nilikuwa nimesimama pale natazama chini pale nilipokuwa nimejilaza kitandani. Huenda nilikuwa nikiota kitandani, lakini nilikuwa hapa juu nikijitazama chini. Unaona? Loo, Yeye alinipa tu safari ndogo ya mwanaanga asubuhi hiyo, akanionyesha mahali pa kwenda. Na inaonyesha kuwa rada yako itaielekeza, mahali ilipo hasa. Sasa, si mimi, ni Yeye. Ni roho yako ndani yako ukiamini Ujumbe huo, na ni Roho Mtakatifu amesimama hapa nilipo, nawe unaiamini hivyo na inawasiliana; na hili hapa linarudi moja kwa moja, jibu lako. Mwanaanga! Amina. Loo, ni ajabu jinsi gani! Naam, bwana.

99 Kubwa, sayansi imefanya jambo kuu. Na, unajua, wamefanya jambo hilo kuu sana mpaka wanajiogopa wenyewe. Hiyo ni kweli. Wana ukuu mwingi hadi wanajiogopa wenyewe. Unajua, walisema hapa yapata miaka miwili iliyopita, ilikuwa "dakika tatu kabla ya usiku wa manane." Wanaogopa. Wanafanya nini? Sasa, mwanadamu ameweza, baada ya asili yake katika mwanaanga wa kawaida, sasa ameweza kufikia mwanaanga huyu. Na anafikiri sasa kwamba wakati Urusi inapoanza kulipua nchi hii, ama nchi nyingine, atasafiri atorekee mwezini.

100 Niliona kitu kidogo kizuri sana hivi majuzi, kilikuwa kizuri sana. Kulikuwa na Wahindi wawili wadogo wamesimama, wakizungumza wao kwa wao, wenye tumbo kiriba, mwajua, namna hiyo, na unyoya nyuma ya kichwa chao, na kupeana tu mkono mmoja na mwingine, wakipigapigana. Kasema, "Dugu, hivi karibuni nchi itarudi kwetu, wazungu wanaenda mwezini." Kasema, "Hivi karibuni nchi yetu itarudi tena. Mzungu anaenda mwezini, kwa hivyo tutakuwa na nchi yetu tena." Ni sawa.

101 Loo, sasa wote wanataka kutengeneza makopo mengi haya ya wanaanga ili waweze kuingia humo. Na e—enzi ya atomiki inakuja, watalipua ulimwengu, wanavuta tu *hii* na wote wanaenda mwezini, kufanya safari ya kwenda mwezini, na kuimaliza, na kwa hivyo watawafanya kuwa uchumi mwingine mwezini. Hawatafika huko. Siamini, kwa moyo wangu wote, watawahi kufika huko. Unaona?

102 Lakini, wakati huo huo, mwaminio halisi wa kweli katika Kristo ameingia Mwanaanga wake. Amina. "Kwa Roho mmoja sote tumebatizwa kuwa Mwanaanga mmoja." Loo, Mwili mmoja! Inaweza kustahimili shinikizo la aina yoyote. Wameijaribu katika tanuru ya moto, itastahimili moto, basi haiwezi kuchomeka; moto mara saba. Wamejaribu katika kila kitu, hutokea sawa. Kwa hiyo wanasayansi wa kiroho wameweza kuthibitisha kwamba wanaweza kustahimili chochote. Kwa hivyo mwa—mwaminio halisi wa kiroho amejipeleka mwenyewe na kuingia ndani ya Mwanaanga wa Mungu, Kristo, akiamini mambo yote; akiweka kando kanuni zake za imani, kanuni za imani za Kipentekoste, kanuni za imani za Kibaptisti, kanuni za imani za Kimethodisti. Ameingia tu katika Mwanaanga, akisema, "Bwana, iko tayari lini?" Loo, jamani! Anafanya nini? Anakuja kwenye mikutano midogo, anasikiliza kuhesabu kinyumenyume kwa Neno la Mungu.

103 Unajua, wakati John Glenn alipoketi pale asubuhi hiyo, walikuwa wakisikiliza kuhesabu kinyumenyume. "Kumi, tisa, nane, saba, sita, tano, nne, tatu, mbili, moja, sufuri." Unaona? Na sasa amefika mahali ambapo inasema, "Ni dakika tatu kabla ya jambo fulani kutukia." Hawajui ni nini. "Dakika tatu hadi tufike saa ya sufuri."

104 Sasa angalia, mwaminio halisi yuko ndani ya Kristo. Hakuna hukumu kwa wale walio ndani ya Kristo. Lihubirini Neno, dumuni moja kwa moja na Neno. Sijali yale madhehebu yasemayo, yataamini Hilo. Watasimama pale pale, kwa maana ni Neno. Madhehebu huanzisha mzozo mkubwa na kuwatenga, kuwafukuza, na kusema "ni wendawazimu," kila kitu namna hiyo. Lakini wao hudumu moja kwa moja na Neno hilo. Mradi tu Mungu aliahidi jambo hilo, wao hukaa hapo kwa sababu wao ni wanaanga. Wanaamini Neno. Na hakuna njia ya kuwaondoa. Watakuacha hata hivyo, kwa hiyo wa—waache tu kwa muda.

105 Bali wako mle ndani, wameketi katika mahali pa Mbinguni katika Kristo Yesu, wakisikiliza kuhesabu kinyumenyume, *Nyakati za Kanisa* na kadhalika. Utukufu! Inakufanya ujisikie vizuri, sivyo? Kusikiliza kuhesabu kinyumenyume! Kuhesabu kinyumenyume ni nini? "Mambo haya yote yaliahidiwa, hapa ndipo yalipotokea. Mambo haya yote yaliahidiwa, hapa ndipo yanapotokea. Ilipo ahadi, hapa ndipo ilipotokea. Mafanikio aliyoahidi leo, haya hapa moja kwa moja miongoni mwetu." Wanafanya nini? Kusikiliza kuhesabu kinyumenyume. Imefikia wapi? Kote kutoka kwa Luther. Kuhesabu kinyumenyume! "Kuhesabiwa haki, utakaso . . . Kumi, tisa, nane, saba, sita, tano, nne, tatu, mbili . . . Panda juu!" Wanafanya nini? Wanasubiri kuondoka, saa ya sufuri. Amina.

[Ndugu Branham, saa nane baadaye, alirekodi sehemu hii ya ziada ya kumalizia iliyoingizwa humu kama aya 106-111. Anafafanua hili wakati wa mahubiri yake ya jioni, *Katika Uwepo Wake*, aya ya 4-5—Mh.]

106 Mzunguko huu mkuu ambao Kanisa linajitayarisha kufanya, na wakati mkuu wa kuhesabu kinyumenyume, Ningependa kukueleza ninachofikiria ni kuhesabu kinyumenyume. Sasa, nafikiri tumepitia tu jambo hilo hapa kanisani. Na sasa unaona ya kwamba, wakati mwanaanga wa kawaida anajitayarisha kuondoka duniani, kuna kuhesabu kinyumenyume kuanzia kumi kurudi hadi sufuri. Sasa, sijajaribu kuchambua Ujumbe huu na kuupatia maana ya kiroho, kwani ingechukua muda mwingi sana asubuhi ya leo. Lakini nataka kujaribu kuwaelezeni hili, kwamba *kumi* ni nambari ya "kiulimwengu," mwanadamu. Lakini *saba* ni nambari ya "ukamilifu wa Mungu." Siku sita aliziumba mbingu na nchi, na ya saba akastarehe. Na miaka elfu sita ulimwengu unapaswa kufanya kazi dhidi ya dhambi, au kanisa kufanya kazi dhidi ya dhambi, na ya saba ni Milenia, Sabato.

107 Saba ni nambari kamili ya Mungu. Na sasa ametupa kuhesabu kinyumenyume sahihi, na kuhesabu Kwake kinyumenyume sio kumi, bali saba. Tumeipitia hivi punde tu katika zile *Nyakati Saba za Kanisa*. Sasa tunaona, na huko katika Ufunuo, kuhesabu kinyumenyume kwa kwanza kulikuwa ni wakati wa kwanza. Kuhesabu kinyumenyume kwa pili, wakati

wa pili. Na kuendelea hadi kuhesabu kinyumenyume kwa saba. Na hapa inaonekana mbele yetu, kama picha inavyochorwa, kwamba tulikuwa na huku kuhesabu kinyumenyume. Nambari ya kwanza iliyohesabiwa ilikuwa Efeso. Nambari ya pili iliyohesabiwa ilikuwa Smirna, Smirna. Kisha Pergamo. Thiatira. Ya tano ilikuwa Sardi. Ya sita ilikuwa Filadelfia. Na ya saba ilikuwa ya Laodikia, wakati wa mwisho wa kanisa. Ndipo ni wakati sufuri, kwa Kanisa kuondoka, baada ya nyakati za kanisa kumaliza muda wao. Sasa, tunajua wakati wa Thiatira umekuja na kupita, na wakati wa Efeso umekuja na kupita, wakati wa Filadelfia umekuja na kupita. Nasi tuko katika wakati wa saba wa kanisa, mwisho wake, wakati wa Laodikia. Na huko ndiko kuhesabu kinyumenyume.

108 Ukiona katika masomo yetu ya awali ya makanisa, alishikilia mkononi Mwake *nyota saba*, ambazo tuliona kuwa ni "watumishi saba wa nyakati saba za kanisa." Kila mmoja wao ametambulishwa kikamilifu kama vile Mungu alivyochukua kuhesabu Kwake kinyumenyume. Tangu wakati alipoondoka, mpaka wakati atakaporudi, anakusanya watu kwa ajili ya Jina Lake. Ilianza Siku ya Pentekoste. Wa kwanza, kanisa la Efeso, nyota na mjumbe wa kanisa hilo tunayeamini kuwa ni Mtakatifu Paulo. Amekuja, na nambari moja imehesabiwa. Wakati wa pili wa kanisa, ambao ni Smirna, ilikuwa ni Ireneo, yule mtakatifu mashuhuri wa Mungu aliyeongoza wakati huo wa kanisa mwishoni. Wakati wa tatu wa kanisa, ambao ulikuwa Pergamo, ilikuwa ni Mtakatifu Columba ambaye alikuwa ni mtakatifu mashuhuri wa Mungu. Wakati wa Enzi ya Giza, katika mateso, wakati wa nne na hesabu ya nne, Mtakatifu Martin wa Tours, mtakatifu mashuhuri kutoka Ufaransa. Wakati wa tano wa kanisa, na mjumbe wake alikuwa Martin Luther kwenye kuhesabu kinyumenyume. Wakati wa sita ulikuwa ni John Wesley kwenye kuhesabu kinyumenyume.

109 Sasa tuko katika wakati wa saba, wakati wa kanisa la Laodikia. Nasi tunamtazamia yule mjumbe mashuhuri wa kutokea mara ya pili kwa Eliya, kwenye kuhesabu kinyumenyume. Na mara huyo atakapotokea, basi ni wakati sufuri na Kanisa linaenda Nyumbani, linapaa angani, kwenda Mbinguni, na kuendelea kupita mwezi, nyota, chochote kile, na kukutana na Yesu.

110 Hii ilitoka wapi na walienda wapi? Ndani ya Mwanaanga huyu. Je, watu waliingiaje kwa Mwanaanga kwanza kabisa? Hivyo ndivyo watakavyolazimika kuingia ndani yake kila mahali, kila wakati. Hiyo ni kweli. Lazima waingie kwa njia ile ile ya kwanza, kwa sababu mzunguko huu mkubwa wa kundi kubwa la watu. Kwamba katika siku za Nuhu, kulikuwa na mlango mmoja tu, na mlango huo ulikuwa mlango pekee wa kuingilia. Kila kitu kinachoingia, haijalishi kama walienda kwenye orofa ya kwanza chini ya kuhesabiwa haki, orofa ya pili,

au orofa ya tatu, wote wanaingia kwenye mlango mmoja. Wote wanaingia kwa njia ile ile.

111 Na ni jambo lile lile katika siku hii ya mwanaanga. Hatuna budi kuingia kwa njia iyo hiyo, tuje kwa njia iyo hiyo, kwa Ujumbe ule ule, kwa Kristo yeye yule, kwa Nguvu zile zile walizopokea Siku ya Pentekoste. Vile vile! Imekuwa ni ile ile wakati wote, kwa maana ni Mlango ule ule. Na tunaingiaje katika mwili huu? Kwa Mlango. Na Yesu ndiye Mlango wa Mwili huu. Kwa hiyo tunaingia na kuzaliwa katika Ufalme wa Mungu, kupitia Mlango, Yesu Kristo. Na sasa Mlango unakaribia kufungwa huko Laodikia, mwisho wa kuhesabu kinyumenyume, nalo Kanisa linajitayarisha kuchukua mzunguko wake juu ya dhiki zote, kila kitu, na kupaa katika mbingu za Mbingu, kulipeleka Kanisa kifuani mwa Mungu. Amina. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Amina.

112 Asubuhi wakati John. . .Glenn huyu aliondoka pale chini, kila mtu alikuwa kifudifudi, akilia na kuomba, akishangaa ni nini atakachoweza kufikia. Na jambo la kwanza, moto ulianza kuenea kutoka kwenye atomi hizo wakati lile kombora kubwa lilipoinuliwa kule Cape Canaveral, likipanda juu hewani namna hiyo, na watu wakipiga mayowe na kulia na kushangaa ni nini kingempata mwanaanga wao aliyekuwa akipanda juu.

113 Loo, lakini Kanisa, utukufu, linaeneza moto fulani pia. Amina. Kuhesabu kinyumenyume kunakuja! Amina! "Kuhesabiwa haki, kutakaswa, ubatizo wa Roho Mtakatifu, wakati wa kanisa la Laodikia," tuko mwisho! Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele! Kuna nini? "Kumi, tisa, nane, saba, sita, tano, nne, tatu, mbili. . .sufuri!" Hawatakuwa wakilia, bali kutakuwa na kuimba na kupaza sauti na kumsifu Mungu, Kanisa linapochukua hatua ya mwanaanga wake kwenda angani ili kuwa pamoja na Yesu Kristo. Amina.

114 Katika mafanikio ya kawaida, wanapelekwa hadi kwenye mwezi. Katika mafanikio ya kiroho tunapaa kuelekea Mbinguni. Amina! Mwanaanga wa kawaida anajaribu kujitafutia mahali kwenye mwezi. Tayari tumeshapata nafasi Mbinguni tayari kabisa. "Nyumbani mwa Baba Yangu mna makao mengi. Nitaenda na kuwaandalia mahali, na nitamtuma Mwanaanga arudi kuwachukua." Kuhesabu kinyumenyume kunaendelea! Je, mnaamini hilo? Amina. Kuhesabu kinyumenyume! "Kumi, tisa, nane, saba, sita, tano, nne, tatu, mbili, moja, sufuri!" Moto unaanza kuenea, huduma inatiwa taji Utukufuni. Haleluya! Na maskini roketi inaanza kupaa, haijaelekezwa mwezini, bali imeelekezwa Utukufuni. Yuko huko mbali, moto wa Mungu unaenea. Nguvu za Roho Mtakatifu zikimwinua juu na kupita mwezi, nyota, kupita chochote ambacho kingeweza kufikiwa na mwanadamu. Kanisa litapaa juu liende kwenye vifua vya Mungu Mbinguni, moja ya asubuhi hizi. Marafiki, mwanadamu ameweza kufikia kile walicho nacho kwa vitu vyake vya

kawaida, na Mungu (nililithibitisha hapa) ameifananisha na ya kiroho.

115 Hebu tuingie ndani ya Mwanaanga, haraka! Milango itafungwa baada ya kitambo kidogo. Kuhesabu kinyumenyume kunaendelea! Sayansi inasema kuhesabu kwao kinyumenyume ni dakika tatu. Yetu inaweza kuwa mbele ya hiyo, inaweza kuwa "moja" tayari kwa "sufuri!" Hebu tuingie. Je, unaamini kuwa kuhesabu kinyumenyume kunaendelea? Na tuinamishe vichwa vyetu basi kwa muda kidogo.

116 Baba! "Kumi, tisa, nane, saba, sita, tano, nne, tatu, mbili . . ." Mungu! "Mataifa yanavunjika. Israeli inaamka, ishara ambazo manabii walitabiri; siku za Mataifa karibu kwisha, zimekumbwa na taabu nyingi; rudini, enyi mliotawanyika, makwenu." Siku ya jinsi gani! Nuru za jioni zinaangaza. Ee Mungu, tunaomba kwamba kila asiyeamini aweke kando mawazo yake yote ya elimu kwa haraka, mawazo yake yote ambayo ni kinyume na Neno Lako, na asubuhi ya leo ataingia katika Mwanaanga huyu mtukufu, kwa sababu tumezaliwa ndani Yake, mle ndani ili kuwa sehemu ya Mwanaanga.

117 Ninaomba, Baba wa Mbinguni, na katika Mwili huu mkuu wa Kristo, kwamba Utawabatiza waaminio leo kwa Roho Mtakatifu. Kidimbwi na kijae watu asubuhi ya leo, wakiungama dhambi zao na kuzikwa katika Jina la Yesu Kristo, na kupanda maskini Mwanaanga, Bwana, ambaye anavuka mwezi na nyota, na kwenda mbali kupita kanuni za imani, madhehebu. Tumemaliza kuhesabu kunyumenyume. Ulituambia kile kingekuwa, zile tatu, hatua hizi tatu za hii. Umezieleza nyakati za kanisa, jinsi zingeenda, wakati wa kwanza wa kanisa, wakati wa pili wa kanisa, wakati wa tatu wa kanisa, wa nne, wa tano, wa sita. Hesabu hii ni saba. Na baada ya saba, wakati huu; tayari tuko ndani yake, wakati wa mwisho wa kanisa. Na sasa kuhesabu kinyumenyume kunaendelea. Nyakati zimehesabiwa, wakati wa Kilutheri, wakati wa Wesley, wakati wa Kipentekoste. Na sasa, Bwana, tukikusanyika ndani ya Mwanaanga, akiwa na kioo kikubwa cha kukuza mbele Zake, tunaweza kuuona Utukufu, kumwona Yesu, kumwona Yeye katika uwezo Wake wote, kumwona katika ahadi Zake zote. Kila kitu alichoahidi kinaakisiwa juu yetu. Tunakushukuru kwa hili.

118 Mungu, naomba kanisa leo liingie haraka katika eneo la usalama, kwani hivi karibuni inakuja saa ya sufuri na mlango wa Mwanaanga mkuu utafungwa, ndege ya Mwanaanga. Nasi tutaenda kama Nuhu alivyofanya alipoingia katika mwanaanga wake, tuseme, alielea ndani na juu ya maji yote ya hukumu. Na, Baba, tunataka kuingia ndani Yako ili tuweze kuelea kupitia vijito vya wakati, kuendelea kupita Mirihi, Jupiter, Venus, juu ya Njia ya Kilimia-Cheupe, kuendelea na kuendelea na kuendelea, ambapo mwanaanga wa kawaida hajui lolote kupahusu. Lakini tunaona ya kwamba unamwacha afanye hivyo kwa ishara, ili

tuwe tayari kwenda. Tunasonga kutoka duniani. Tujalie, Bwana. Kupitia Jina la Yesu Kristo, ninaomba.

119 Hapa zimewekwa leso, Bwana, zimewekwa hapa, ambazo wagonjwa wametuma. Wanaamini, Bwana. Na jalia wawe wanaanga kamili asubuhi ya leo. Jalia uweza wa Mwenyezi Mungu anayeiakisi Biblia Yake juu ya hili, kwamba walichukua kutoka kwenye mwili wa Mtakatifu Paulo, leso na nguo, na wagonjwa na wanaoteseka waliponywa. Jalia huyo mwaminio mwanaanga, hiyo ikimgusa, aondoke, Bwana. Ugonjwa nyuma! Jalia kila mgonjwa hapa sasa hivi, Bwana, aingie moja kwa moja ndani ya Kristo Yesu, kwenye Neno Lake, ahadi Yake. Na kusema, "Mwombeni Baba lolote katika Jina Langu, nitalifanya." Jalia waanze kuhesabu, "Kumi, tisa, nane, saba, sita, tano, nne, tatu, mbili . . . sufuri. Waondoke, Bwana!" Jalia wainuke kutoka kwenye vitanda, machela, chochote kile. Na wainuke kutoka katika ugonjwa wao uliowafunga, kwenda huko nje katika anga za juu ambako sayansi ya madaktari, hakuna hata mmoja wao, anayejua lolote kuzihusu, ambapo Nguvu za Mungu zimeahidi kwa utafiti wa kisayansi wa Biblia hapa, au utafiti wa kiroho, hasa, wa Biblia; kuonyesha kwamba Mungu daima amekuwa Mungu, angali Mungu, daima atakuwa Mungu, naye ni Yule Asiye na kikomo, Mwenye nguvu zote, Mwenyezi, Aliyepo Pote ambaye anaweza kulitimiza Neno Lake; na anaweza kufanya mambo yote, na akatuahidi mambo yote yanawezekana kwa wale watakaoamini. Mungu, tujalie.

120 Jalia huyo mwanamume au mwanamke mpotovu, mvulana au msichana, asubuhi ya leo, ambaye hayuko mle ndani akisikiliza kuhesabu kinyumenyume kwa Neno la Mungu, tukijua ya kwamba tuko chini kabisa, tayari tumehesabu jambo la mwisho. Yuko tayari kupiga kelele "sufuri" wakati wowote, na kanisa kwenda. Tunaona Ujumbe ukiisha. Tunaona mateso yakiinuka, kama tulivyozungumzia jana usiku. Tunajua kwamba wakati umekaribia. Kuhesabu kinyumenyume kumekwisha. Umetusaidia hapa jukwaani kuzileta nyakati za kanisa, na kuchukua kila kitu kingine na kuthibitisha, kwamba sasa hivi wakati wowote inaweza kutokea. Mwenyezi Mungu, Yeye aliyeziumba mbingu na nchi, tuma rehema Zako kwa watu na uwape ulichowawekea akiba. Kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu.

121 Na kila mwanaume na mwanamke wakiwa wameinamisha vichwa vyao. Ikiwa kuna wengine hapa ambao hawamjui Kristo kama Mwokozi wao asubuhi ya leo, na wangependa kumjua na kuingia katika hali hii ya Mwanaanga ya neema ya Mungu, kwenda katika Unyakuo, naomba uinue mkono wako na kusema, "Niko tayari, ninataka kuwa tayari kwa Unyakuo, Ndugu Branham. Niombee." Mungu akubariki. Mungu akubariki, wewe. Mungu akubariki, na wewe. Nje, ndani, popote ulipo, inua tu mkono wako. Kwa huu, sema, "Mungu, niingize ndani."

Mungu akubariki. "Nataka kusikia kuhesabu kinyumenyume. Nataka kukusikia. Ninataka kujua kuwa niko salama, kwamba moto utakapozimika sitakuwa nimeketi hapa chini kwenye gari la kukokotwa na farasi. Sitakuwa kwenye kanisa, nikiendesha motokaa. Sitakuwa katika moja ambayo inaweza tu kuinua miguu yake kutoka ardhini sasa, kwa muda wa kutosha kuruka na kuwa na kelele nyingi. Ninataka kuwa katika kitu ambacho kitanipeleka kupita mwezi na nyota. Ninataka kusikiliza kuhesabu kinyumenyume; si kanuni fulani ya imani, madhehebu fulani. Lakini ninataka kuwa ndani ya Kristo, ambapo ninaweza kusafiri kupita chochote ambacho ni hoja miongoni mwa wanadamu. Nataka kwenda."

122 Je, kuna mwingine kabla hatujaomba? Je, kuna . . .? Mungu akubariki, msichana. Mungu akubariki, kijana mwanaume. Mungu akubariki, na wewe huko nyuma. Ninauona mkono wako, na bila shaka Mungu anauona. Na wewe, ndugu yangu, wewe ndugu. "Nataka kuwa katika kuhesabu kinyumenyume. Mungu, nijalie niweke kando kila mzigo." Mungu akubariki, ndugu. "Nataka kuweka kando kila dhambi. Nina hasira Ndugu Branham. Loo, nisingeweza kuingia katika Huo namna hiyo. Omba Mungu aniondolee. Mimi—mimi, Ndugu Branham, mimi—mimi hunywa kidogo. Sitaki kufanya hivyo. Omba kwamba nitaiweka kando. Ninavuta sigara. Sitaki kufanya hivyo. Mungu anajua sitaki kufanya hivyo. Jambo hilo limenifunga tu hivyo, mimi—mimi huvuta sigara tu, siwezi kabisa kuziacha. Najua ni makosa, na sipaswi kuifanya. Sitafanya! Jambo lingine, nimekuwa nikilititilia shaka Neno. Nimekuwa tu nikijiuliza kama Hilo kweli ni sahihi. Nisaidie, Mungu. Nijalie, nijalie tu kukumbuka yote ni kweli, nami ninaamini Hilo. Nataka kusikiliza kuhesabu kinyumenyume. Ninataka kufika mahali ambapo kila wakati ninapoona Neno la Mungu likisema chochote, ninataka kuliitikia kwa 'amina' na kusema 'Ni Wewe, Bwana.'" Sasa wote . . . Mungu akubariki. Mungu awabariki, kila mmoja wenu.

123 Kuna wengine hapa ambao ni wagonjwa, na kusema, "Ndugu Branham, asubuhi ya leo mimi ni Mkristo, lakini mimi . . . Nimekuwa . . . nimepata Roho Mtakatifu. Nimeshuka kwenye ndege sasa, niko tayari kwa kuhesabu kunyumenyume. Nimetoka katika kila aina ya madhehebu na chochote kile, nikisikiliza kuhesabu kinyumenyume. Lakini sasa nataka kusema jambo hili moja, Ndugu Branham, asubuhi ya leo, mimi ni mgonjwa. Nina kazi ya kufanya kwa ajili ya Bwana bado. Ninasikiliza kuhesabu kinyumenyume, lakini nataka—nataka kuwa mzima. Ninapanda juu yake asubuhi ya leo, kusikiliza kuhesabu kinyumenyume." Kuhesabu kinyumenyume ni nini? Neno la Mungu. Inahesabiwa ikirudi nyuma moja kwa moja. Ni yeye yule jana, leo, na hata milele. "Ninataka kumsikia kama Mponyaji wangu asubuhi ya leo. Nataka kuinua mkono wangu

na kusema, 'Niombee, Ndugu Branham.'" Mungu akubariki. Ingia sasa hivi. Ingia moja kwa moja ndani. Madhabahu imejaa, na kote hapa, wamelundikana sakafuni. Hatungeweza kuendesha mstari wa maombi. Wanasimama karibu na kuta na kila kitu. Tuna msongamano tu. Haitupasi kufanya hivyo. Uko katika—uko katika . . . Wewe ni mwanaanga.

124 Wewe ni mwanaanga. Unaenda kupita Luther. Luther haamini katika hayo yote. Wesley aliweka mikono. Wapentekoste wanapaka mafuta. Wewe ni mwanaanga, umeenda kupita hoja yoyote. Kwa sababu tu Neno lilisema hivyo, ninaendelea. Vema, unasema, "Kwani Luther hakuamini? Kwani hilo halikuwa Neno?" Naam, lakini Wesley alienda zaidi yake. "Vema, Wesley alipaka mafuta ama kitu kingine. Je, huamini hivyo?" Naam, hiyo ni kweli. "Wapentekoste walitoa pepo." Ndiyo. "Aliwekewa mikono, alikuwa na uponyaji mikononi na chochote kile." Ndiyo, najua hiyo ni kweli, lakini endelea. Endelea! Wesley hatazami nyuma kwa Luther, Pentekoste haitazami nyuma kwa Wesley. Wala hatuangalii nyuma kwenye Pentekoste. Sisi ni wanaanga. Tumeenda zaidi ya hapo. Hebu tuendelee. Kristo alisema hivyo!

125 Je, unafanyaje? "Njoo uweke mikono yako juu ya binti yangu naye atapona," alisema Myahudi. Yesu alienda na kufanya hivyo kwa ajili yake, hiyo ni kweli. Lakini ilipofika kwa Mrumi, mwanaanga, alisema, "Sistahili Wewe kuja chini ya paa langu. Sema tu Neno, Bwana." Na Yeye tayari amesema. Ndilo hilo.

126 Sasa hebu tuinue mi—mioyo yetu kwa Mungu. Hebu tuinue mikono yetu kwa Mungu, mioyo yetu kwa Mungu. Kwa kuwa chochote unachohitaji, wokovu, utakaso, ubatizo wa Roho Mtakatifu, uponyaji wa Kiungu, chochote kile, inua mikono yako na ushikilie moyo wako moja kwa moja katika Uwepo wa Mungu, na utambue ya kwamba umeketi katika mahali pa Mbinguni katika Kristo Yesu, nawe ni mwanaanga wa Imani hiyo. Nini? Hii hapa inakuja hesabu! "Kumi, tisa, nane, saba, sita, tano, nne, tatu, mbili . . ." Ee Yesu, njoo sasa! Tunaweka nguvu za Jina Lake. Na kama tulivyoona jana usiku, Paulo alimpiga mtu kwa upofu, akamwacha mwingine amkanyage. Na tunaona kwamba Yesu angeweza kufanya chochote ambacho Yeye—Yeye alifanya, kila aina ya miujiza, na hata hivyo alikuwa papo hapo mwisho wa safari Yake, akiona alibwagwa chini na kutemewa mate, na chochote kile. Watu hawaelewi. Wanatambua ya kwamba Mungu anafanya hivyo ili kuthibitisha ya kwamba ni kweli, na kisha anaijaribu imani ya watu.

127 Bwana, tumesimama hapa na kuona vipofu kabisa wakipokea kuona kwao, magonjwa; kansa ambao walikuwa kivuli cha watu, ziliponywa. Tumewaona wale ambao walikuwa wamekufa na kulazwa kwa masaa baada ya masaa, na kufufuka tena. Tunajua kwamba hilo—hilo ni Kristo wetu mkuu ambaye kwake sisi ni mwanaanga katika mwili Wake. Na sasa kuhesabu

kinyumenyume kunaendelea, nasi tutaamini asubuhi ya leo kwa ajili ya uponyaji wetu, kwa ajili ya wokovu wetu, na kwa kila kitu tunachohitaji. Kwa sababu tunapoomba katika Jina la Yesu Kristo, Yeye aliahidi, "Mwombeni Baba Yangu neno lolote katika Jina Langu, nitalifanya." Na hilo ndilo tu tunalohitaji kufanya sasa ni kuliita Jina Lake, na halina budi kufanywa. Tunasikiliza kuhesabu kinyumenyume.

128 Bwana, baadhi yao ambao wamekuwa wenye dhambi, waliinua mikono yao. Wanangojea kuhesabu kinyumenyume, wakati kutakuwa na mabadiliko katika moyo wao, hiyo itaondoa maskini ufisadi mbaya wote. Kuna wengi wanaovuta sigara, ambao wako tayari kuziweka chini. Wengi ambao wamefanya mambo ambayo hawakupaswa kufanya, na wako tayari kuyaweka chini, kwa sababu tunamwomba Mungu Mwenyezi katika Jina la Yesu Kristo kuondoa kila kitu kinachozuia Kanisa asubuhi ya leo, kuanzia ugonjwa hadi dhambi, na kuliacha kanisa hili liwe huru. Katika Jina la Yesu Kristo, naomba uweza na Nguvu za Injili kuu, Moto wa Roho Mtakatifu uanze kutawanyika, na wanaanga wakuu wa Mungu waondoke kwa shauku ya mioyo yao leo hii. Tujalie, Mwenyezi Mungu. Wao ni Wako. Na jalia wapokee uponyaji wao, wokovu wao, na chochote wanachohitaji. Ninawaleta Kwako, na kuwakabidhi Kwako kwa maombi yangu, juu ya madhabahu ilipo Damu ya Yesu Kristo asubuhi ya leo. Katika Jina la Yesu Kristo na wapokee walichoomba.

Na watu wakasema, "Amina." [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.].

129 Kwa hiyo, liamini! Iwe hivyo! Ninaliamini. Naamini. Amina. Ninajua ya kwamba Yeye ni Mungu. Ninajua kuwa tuko tayari kwa mafanikio makubwa ya Mungu. Mafanikio yake ni yapi? Kuondoka duniani. Mwanaanga huenda kwenye mwezi, dunia nyingine. Nalo Kanisa la Mungu (kutoka kwa ndege, kutoka kwa mgongo wa farasi na kadhalika) anaondoka kama mwanaanga, kwenda kwenye ulimwengu mwingine, ambao ni Mbinguni. Kuhesabu kinyumenyume, kunaendelea. Amina.

Mnampenda? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Basi na tuinue mikono yetu na kuimba.

> Nampenda, nampenda
> Kwani kwanza . . .

Vema, Ndugu Neville.

Bwana asifiwe! Na Mungu awabariki mpaka usiku wa leo nitakapowaona.

*KUHESABU KINYUMENYUME*   SWA62-0909M
(Countdown)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza Jumapili asubuhi, tarehe 9, Septemba, 1962, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2023 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:



Voice Of God Recordings

P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.

www.branham.org